Leo yetu ndiyo kesho yetu

# Uelekeo

UMG Kazi na Utuvu

Uongozi na wafanyakazi wa
Uhuru Media Group
wanawatakia wafanyakazi wote
maadhimisho mema ya
Siku ya Wafanyakazi

## Je; kuna ukweli wowote kuku wa 'kizungu' wana madhara kiafya?



Uk. 7

## Mei Mosi 1995 Nyerere alitaka kiongozi kaliba ya Rais wa sasa



Uk. 12



## Unapolalamikia maisha magumu wewe binafsi umechangiaje?

Uk. 14

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00063 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Mei 1 - 7, 2024 |

## TIC kujenga ofisi Arusha



Na Mwandishi Wetu, Arusha

KITUO cha Uwekezaji Nchini (TIC), kinatarajiwa kujengwa ofisi mkoani Arusha ili kupanua huduma kwa wadau wanaotaka kuwekeza katika sekta ya utalii na nyinginezo.. Uk . 4

## Warioba: Waandishi fanyeni tafiti



Uk. 2

## Mwenge wa Uhuru watoa kauli kwa watendaji

Na Mwamvua Mwinyi, Bagamoyo

KIONGOZI wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Godfrey Mzava, amewataka watendaji kuendelea kumsaidia Rais Dk. Samia Suluhu Hussam katika jitihada... Uk. 3

### MAADHIMISHO MEI MOSI:

# Wafanyakazi wote leo masikio kwa Rais Samia






## ... Azidi kuungwa mkono matumizi ya nishati safi

Uk. 2

# Rais Dk. Samia azidi kuungwa mkono matumizi ya nishati safi

**Na Hellen Mwango**

KAMPUNI ya Orxy Tanzania, imegawa mitungi 100 ya gesi ya kupikia kwa wahariri na waandishi wa habari kama sehemu ya jamii ikiunga mkono uhamasishaji unaofanywa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Orxy Tanzania, Benoite Araman, alisema kampuni yake imeipa umuhimu mkubwa kampeni ya Rais Dk. Samia kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Alisema wahariri na waandishi wa habari, wana nafasi kubwa ya kutoa elimu na kufikisha taarifa haraka kwa jamii.

"Kampeni hii tunaipa uzito mkubwa kutokana na nafasi yenu katika jamii kwa hiyo kupitia mitungi hii mtafikisha kwa haraka zaidi umuhimu wa kuachana na matumizi ya kuni na mkaa na kujikita kwenye nishati safi.

"Pia, tunajikita katika kumuondolea mwanamke na msichana wa Kitanzania, maradhi ya mara kwa mara yanayotokana na kuvuta moshi wa kuni na mkaa," alisema.

Alisema imeweka kipaumbele katika kuhamasisha nishati safi ya kupikia na wameamua kuibeba kampeni hiyo kwa ukubwa wake.

Alisema wako sambamba na serikali hasa Rais Dk. Samia kuhakikisha dhamira yake ya kufikisha asimilia 80 ya matumizi ya nishati safi ifikapo 2030 na kwamba Oryx imedhamiria kutimiza ndoto hiyo.

"Tunawakabidhi mtungi wa gesi kilo 15 na jiko lenye sehemu mbili za kupikia, ninyi ni kundi lenye ushawishi mtahamsisha jamii kutumia nishati safi kwa haraka zaidi, kwa nafasi zenu mnashiriki matukio mbalimba ya mabadiliko hayo tunawashukuru sana waandishi wote," alisema.

Mpaka sasa Oryx wametoa mitungi 33,000 katika makundi na maeneo mbalimbali Bara na Visiwani yenye thamani ya Sh. bilioni 1.5.

Akizungumzia faida wa taasisi kutumia gesi, alisema kuna faida kubwa na kwamba inasaidia kuongeza ufanisi na kupunguza muda wa kutafuta nishati nyingine kama kuni na mkaa pamoja na kulinda mazingira kwa kutokomeza ukataji wa miti.

Faida nyingine ni kuwaepusha wanawake na watoto kupata majeraha wakati wa kubeba kuni na mazingira hatarishi ya kukutana na wanyama wakali wakati wakitafuta kuni na watapata muda wa kufanya shughuki za uzalishaji wa kiuchumi.

Alisema ili kufanikisha kampeni hiyo na kuhakikisha kila Mtanzania anatumia gesi bila kujali kipato, wanashirikiana na NMB kwa ajili ya kufanya malipo ya kununua gesi kidogo kidogo ama kibubu.

Kwa upande wake Meneja Usambazaji, Peter Ndomba alisema matumizi ya gesi yanahitaji uangalifu ikiwamo kuzuia watoto kuwa karibu au kuchezea sehemu ya mfuniko wa mtungi ili kuepusha matukio ya ajali ya gesi.

"Gesi huwa ni hatari kama itawekwa kwenye mazingira yasiyo mazuri lazima kuwe na sababu ya kulipuka, haiwezi kusababisha ajali kizembe, inahitaji uangalifu mkubwa hasa kwa watoto.


"Kwa mfano, mtu unachoma nyama na jiko la mkaa pembeni ya mtungi wa gesi hiyo ni hatari, wale wanaojaza bila kufuata utaratibu, kinyume cha sheria gesi ni hatari pia," alisema.

Alisema Tanzania ina nyumba milioni 14 wanaotumia gesi milioni mbili lengo ni kufikiwa watu milioni nane wanaotumia nishati safi.



Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Oryx, Benoite Araman, akimkabidhi mtungi na jiko la gesi Mpigapicha Mkuu wa Magazeti ya The Guadian Ltd, Selemani Mpochi, ikiwa ni kuunga mkono kampeni ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ya matumizi ya nishati safi. (Picha: Mpigapicha Wetu).

# Warioba: Waandishi fanyeni tafiti kuisadia serikali kutoa maamuzi



Jaji Joseph Sinde Warioba

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

WAANDISHI nchini, wametakiwa kulisaidia taifa kwa kufanya tafiti zitakazoisaidia serikali kutoa maamuzi ikiwamo kuendeleza nchi na kuzitumia katika kuielimisha jamii.

Rai hiyo ilitolewa jana na Waziri Mkuu wa zamani Jaji Joseph Warioba, wakati akifungua kongamano la Baraza la Habari Tanzania (MCT) la wadau wa habari na uchaguzi jijini Dodoma.

"Vyombo vya habari vinaandika na kutangaza habari za matukio zaidi bila kuzingatia mojawapo ya misingi yake mikuu mitatu, ikiwamo kuelimisha," alisema.

Alisema umuhimu wa vyombo vya habari kufanya utafiti, kuelimisha jamii na kuishauri serikali kuhusu matokeo ya tafiti hizo.

"Wanahabari, msiwe sehemu ya kulalamika wakati mna nafasi ya kutengeneza ajenda kwa kufanya utafiti na kutoa elimu ya mambo ya msingi kwa nchi," alisema Jaji Warioba.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Idara ya Habari Tanzania (Maelezo) na Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, aliipongeza MCT kwa kuandaa kongamano hilo na mchango wake katika kuboresha weledi, maadili na uwajibikaji kwenye tasnia ya habari.

Alisema MCT inasaidia katika kuboresha viwango vya kazi za uandishi na utangazaji wa habari nchini, ikiwamo kutetea haki za wananchi pamoja na waandishi wa habari.

Aidha, alisema anavishukuru vyombo vya habari kwa kazi kubwa na nyeti wanayoifanya ya kuuelimisha umma, hasa katika kipindi cha Uchaguzi.

Hata hivyo, alivikumbusha vyombo hivyo nchini kuzingatia uandishi wa habari za kweli, zilizo sahihi na zinazozingatia mizania.

Alionya kuwa uandishi na usambazaji wa habari za uongo si tu zinafifisha taswira ya nchi na ya fani ya uandishi wa habari, bali pia kwa mwandishi na vyombo vyao.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji MCT, Ernest Sungura, alisema vyombo vya habari vya Tanzania huwa havina maandalizi ya pamoja ya namna ya kuandika na kutangaza habari za uchaguzi.

"Vyombo vya habari nchini, havina maandalizi katika kila hatua ya mchakato wa uchaguzi kuanzia uboreshaji wa daftari la wapiga kura, kujiandikisha kwa wapiga kura, uteuzi wa wagombea, elimu kwa mpiga kura na kampeni hadi siku ya kupiga kura," alisema.

Alisema vyombo vya habari nchini wakati wote vinajikita katika maneno ya wana siasa na mambo binafsi ya wagombea badala ya kujikita katika kuelimisha na kutoa taarifa sahihi za masuala ya msingi na mambo yanayowaathiri wananchi katika maisha yao ya kila siku.

"Vyombo vya habari nchini huwa havina uelewa mpana wa viwango vya kimataifa vya masuala ya uchaguzi, sheria na kanuni mbalimbali za uchaguzi Tanzania," alisema.

Alisema mambo mengine ni pamoja na mifumo ya usimamizi wa uchaguzi, uelewa mpana wa sera, itikadi ya vyama vya siasa na ilani zao za uchaguzi.

Kaulimbiu ya kongamano hilo la wadau wa Habari na Uchaguzi Tanzania ni 'Uandishi wa habari za uchaguzi kwa weledi hujenga usawa, haki na uwajibikaji.'

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, Katibu ya Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, CPA Amos Makalla, alisema chama chake kitakuwa mstari wa mbele kutekeleza kwa vitendo haki, usawa na wajibu ili kuwa na uchaguzi ulio huru, wa haki na wenye kuaminika.

Alisema anavikumbusha vyombo vya habari kuwa pamoja na kuandika habari zao kwa uhuru, lakini wanapaswa kutambua kuwa hawana nchi mbadala hivyo ni muhimu kuhakikisha habari zote zinaiacha nchi ikiwa salama na yenye amani.

# Mwenge wa Uhuru watoa kauli kwa watendaji





**Na Mwamvua Mwinyi, Bagamoyo**

KIONGOZI wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Godfrey Mzava, amewataka watendaji kuendelea kumsaidia Rais Dk. Samia Suluhu Hussam katika jitihada zake madhubuti za kuwaletea wananchi maendeleo na kuinua uchumi wa Taifa.

Alisema hayo wakati akikagua na kuweka jiwe la msingi katika mradi wa upanuzi wa maji, ujenzi wa tangi la maji lita 50,000 Kijiji cha Kidomole, Halmashauri ya Bagamoyo mkoani Pwani jana.

Mradi huo utakaogharimu Sh. milioni 176, umefikia asilimia 90 na utahudumia kaya 700 zenye wakazi 3,660.

"Maji hayana mbadala, kila siku lazima tuguse maji, kwa umuhimu huo, Rais Dk. Samia anaendelea kuboresha miundombinu ya maji, kushusha fedha kwenye miradi ya huduma, kujenga miradi ya maji ilihali wananchi wapate huduma na maji safi, salama yenye uhakika na karibu na mazingira yao ili wasifuate umbali mrefu.

"Miradi yote ya maendeleo isimamiwe na muendelee kushirikiana Chama Cha Mapinduzi (CCM) na viongozi wa Serikali ili mambo yaende vizuri, nimeona ushirikiano ulipo sasa, endelezeni kwa manufaa ya jamii," alisema.

Alisema Rais Dk. Samia yupo tayari na amekuwa na utashi kuhakikisha anashusha rasilimali fedha kutatua kero za wananchi ikiwemo kusogeza huduma ya maji safi, salama na karibu ya jamii.

Akipokea Mwenge wa Uhuru katika viwanja vya Shule ya Msingi Fukayosi, Kata ya Fukayosi kutoka Halmashauri ya Chalinze, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Bagamoyo, Shauri Selenda, alisema miradi 15 yenye thamani ya Sh. bilioni 13.7 itatembelewa na kukimbizwa urefu wa kilomita 159.7.

Miradi mingine iliyotembelewa na Halmashauri ya Bagamoyo ni kukagua mradi wa duka la dawa za jamii, Hospital ya Wilaya na mradi wa barabara, Kitongoji cha Benki, Kata ya Dunda.

Pamoja na hayo, umekagua shughuli za makundi yenye mahitaji maalum na ukatili wa kijinsia, kukagua mradi wa sekta ya barabara, sekta ya elimu, afya 2024 na kukagua shughuli za uhifadhi wa mazingira na uchakataji wa mifuko ya sandarusi.

# Takukuru yaanza na elimu utekelezaji miradi ya umma

**Na Mwandishi Wetu, Mwanza**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Mkoa wa Mwanza, katika kuzuia vitendo vya rushwa kwenye miradi ya maendeleo, imeanza na mkakati wa kutoa elimu kwa wananchi kusimamia matumizi ya sahihi ya fedha zinazotolewa na serikali ili kutekeleza miradi hiyo.

Pia, katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2023/24, itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kuchunguza makosa ya rushwa na kuwachukulia hatua watakaojihusisha na vitendo vya rushwa kwa mujibu wa sheria.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Mwanza, James Ruge, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu taarifa ya utendaji wa taasisi hiyo katika kipindi cha Januari hadi Machi, mwaka huu.

Alisema katika robo ya nne ya mwaka 2023/24, imeandaa mkakati wa kuzuia vitendo vya rushwa kwa kuwaelimisha wananchi kusimamia kwa karibu zaidi matumizi ya fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.




**Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mwanza, James Ruge, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani), jana alipokuwa akitoa taarifa ya utendaji wa taasisi hiyo kwa kipindi cha Januari hadi Machi, mwaka huu.**

Alisema mbali na kutoa elimu ya kuzuia vitendo vya rushwa na madhara yake katika jamii, wataendelea kutekeleza majukumu yao ya kuchunguza makosa ya rushwa na kuwachukulia hatua wale wote watakaohusika na vitendo hivyo kwa mujibu wa sheria.

"Takukuru Mwanza inatoa wito kwa wananchi kusimamia miradi ya maendeleo inayotekelezwa na serikali katika maeneo yao. Kwa pamoja tuzuie na kukemea vitendo vya rushwa katika maeneo ya kupata huduma kwa kuwa ni jukumu letu sote wananchi," alisema.

Mapema, Ruge alisema wananchi wa maeneo mbalimbali mkoani Mwanza, wamefurahia na kunufaika kwa kupata huduma bora za afya, maji, umeme, elimu na barabara kutokana na utekelezaji wa programu ya Takukuru Rafiki.

"Programu hiyo inayolenga kutambua kero katika sekta ya huduma za jamii na miradi ya maendeleo katika sekta za maji, elimu, nishati ya umeme, afya, ardhi na barabara imekuwa na manufaa kwa wananchi katika uboreshaji wa huduma," alisema.

Alisema katika kipindi cha Januari hadi Machi, mwaka huu, manufaa mengi yamepatikana kupitia programu hiyo ya Takukuru Rafiki na manufaa kama vile kutengenezwa kwa pampu ya maji na kuwezesha wananchi wa Kata ya Mahina wilayani Nyamagana, kupata huduma maji sasa.

# Wafanyakazi wote leo masikio kwa Samia

**Na Mwandishi Wetu**

LEO ni Mei Mosi ambayo ni siku maalum kwa wafanyakazi kote duniani ambapo nchini Tanzania, maadhimishio ya kitaifa yanafanyika jijini Arusha na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ni mgeni rasmi.

Macho na masikio ya wafanyakazi nchini, leo yameelekezwa kwa Rais Dk. Samia kusikiliza atakavyoijibu kaulimbiu ya mwaka huu ya Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi nchini (Tucta) inayosema "Nyongeza ya mishahara, ni msingi wa mafao bora na kinga dhidi ya hali ngumu ya maisha."

Katika mkutano wake na waandishi wa habari hivi karibuni, Rais wa Tucta, Tumaini Nyamhokya, alisema kaulimbiu hiyo inaendana na uhalisia wa maisha ya mfanyakazi kwa sasa kwani gharama za maisha zimepanda na mishahara haikidhi mahitaji ya kila siku ya mfanyakazi.

Kadhalika, alisema mishahara ikiwa bora, itawezesha pia mafao kuwa bora wakati wa kustaafu.

Nyumhokya alisema maadhimisho ya Mei Mosi mwaka huu, yameratibiwa na vyama vyote 13 vinavyounda Tucta.

Alivitaja vyama hivyo kuwa ni Chodawu, COTWU (T), CWT, Dowuta, Raawu, TALGWU, Tamico, Tasu,, Tewuta, TRAWU, TPAWU, Tughe na Tuico .

Aidha, alisema Tucta imeshirikiana na vyama vyote vilivyo nje ya shirikisho hilo vilivyojitokeza katika maandalizi hayo.

Tayari Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, ametoa wito kwa wananchi kujitokeza kwa wingi kushiriki kilele cha siku hiyo ya wafanyakazi yanayofanyika katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid Kaluta ambapo Rais Dk. Samia ni mgeni rasmi.

Alitoa wito huo hivi karibuni alipokuwa azungumza kwenye kikao kazi cha maandalizi kuelekea Siku ya Wafanyakazi Duniani kilichofanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

Alisema uwepo wa shughuli hiyo ya kitaifa mkoani humo, ni fursa kubwa kwa wakazi wake katika kuchangamkia fursa, hivyo uongozi wa mkoa huo umeandaa eneo maalumu kando ya uwanja wa Sheikh Amri Abeid kwa ajili ya kutumiwa na wajasiriamali kufanya biashara zao.

Alisema uwepo wa siku ya wafanyakazi unaashiria uhuru na haki za wafanyakazi mahala pa kazi.

Alisema ni vyema wananchi wakatambua kuwa ushiriki wao utawaongezea morali watumishi katika kuhudumia jamii, hivyo wajitokeze kwa wingi kuhudhuria siku hiyo maalum ya wafanyakazi.




# TIC kujenga ofisi Arusha

**Na Mwandishi Wetu, Arusha**

KITUO cha Uwekezaji Nchini (TIC), kinatarajiwa kujengwa ofisi mkoani Arusha ili kupanua huduma kwa wadau wanaotaka kuwekeza katika sekta ya utalii na nyinginezo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo, alisema hayo jijini hapa jana wakati akitoa hotuba ya ufunguzi wa Kongamano la Uwekezaji kwenye Sekta ya Utalii lililohudhuriwa na zaidi ya wadau 420 kutoka serikalini, wadau wengine kutoka ndani na nje ya nchi.

Alisema kupitia utekelezaji wa sera na sheria mbalimbali za uwekezaji na maelekezo ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, serikali imeendelea kupata mafanikio katika kuhamasisha, kuvutia na kuwezesha uwekezaji nchini.

Profesa Mkumbo alitaja mambo 10 ya msingi katika utalii ikiwemo amani, utulivu na salama, malazi, miundombinu ya usafiri, mikakati mizuri ya kutangaza utalii, suala la tabia njema na ukarimu wa wenyeji.

Mengine ni uwepo wa miundombinu ya malazi, elimu kwa watoaji huduma kwa watalii, uwepo wa mitaji kwa ajili ya uwekezaji, uwepo wa idadi ya watu wenye uwezo wa kuongea lugha zaidi ya moja, kuwepo na vituo vya kujifunza lugha na uhusiano bora wa kimataifa.

Akizungumza katika kongamano hilo Waziri wa Maliasili na Utalii Angela Kairuki (Mb) alisema kutokana filamu ya The Royal Tour wameweza kufikia watalii milioni 1.8 na wanajianda zaidi kuona namna ya kuongeza watalii na maeneo ya malazi ikiwemo kuandaa malazi ya madaraja mbalimbali yenye ubora, usafi pamoja na huduma zinazopatikana

"Fursa bado zipo katika mnyororo wa thamani ambapo kwa umoja wetu utatusaidia kuboresha uchumi zaidi na kuongeza pato ila lengo likiwa ni kufikia matarajio ya watalii wanapokuja wapate kumbukumbu nzuri sambaba na wenyeji wasiwe 'ndugu watazamaji' na badala yake wawe wa moja katika kuongezea Pato la Taifa.

"Tunatakiwa kuongeza utalii wa mikutano kwa kuhakikisha ukumbi wa AICC unakamilika kwa haraka ili uwe na tija, wageni wavutiwe zaidi pamoja na kuliongezea Taifa kipato," alisema.

Akieleza Maudhui ya mkutano huu, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Dk. Tausi Kida, alisema kongamano hilo ni takwa kutoka ofisi hiyo ambayo Rais Dk. Samia aliitoa wakati akiwaapisha viongozi.

Aidha, alisema utalii wa ndani unaongezeka kwa kasi hadi kufikia watu milioni 1.9 tofauti na hapo awali, kwani mwaka 2022 Tanzania ilikuwa inapokea watalii 1.5 milioni ukilinganishwa na mwaka 2023 watalii wameongezeka hadi kufikia milioni mbili alisema kwa sasa Tanzania inapokea wageni milioni nne huku changamoto ya vidanda ikiwepo132, 676.



**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo**

# TAEC yapunguza muda wa utoaji cheti cha uchunguzi wa mionzi

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Nguvu za Atomu Tanzania (TAEC), imepunguza kwa asilimia 98 siku za utoaji wa cheti cha uchunguzi wa mionzi (RAC) kutoka zaidi ya siku saba hadi kufikia kwa wastani wa saa tatu hadi siku moja.

Awali, utaratibu wa uchunguzi wa mionzi ulikuwa una mlolongo mrefu na kusababisha malalamiko mengi kutoka kwa wadau mbalimbali ambapo mfumo wa kielektroniki umesaidia mno.

Hayo yalisemwa jijini Dar es Salaam juzi na Mkurugenzi Mkuu wa TAEC, Profesa Lazaro Busagala,



Mkurugenzi Mkuu wa TAEC, Profesa Lazaro Busagala

> **Serikali imejenga majengo sita ya maabara na ofisi katika kanda tano yenye thamani ya takribani Sh. bilioni 28.11 ambapo majengo manne kati ya hayo, yamekamilika. Miradi hiyo ipo Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Mwanza na Zanzibar.**

alipokuwa akiwasilisha kwa wahariri na waandishi wa vyombo vya habari chini ya uratibu wa Msajili wa Hazina, Nehemiah Msechu, mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kupitia TAEC.

Aidha, Profesa Busagala alisema Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwan na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imeondoa tozo na kupunguza tozo kwa kuamua kubeba gharama za upimaji hususan kwa wale wanaosafirisha bidhaa nje ya nchi kwa kupunguza kutoka asilimia 0.2 ya malipwani kuwa asilimia 0.1 ya malipwani, sawa na punguzo la asilimia 50.

Hali kadhalika, alisema kwa wafanyabiashara wadogo, hupatiwa bure huduma ya upimaji wa sampuli sawa na punguzo la asilimia 100.

Vile vile, Profesa Busagala alisema serikali imeendelea kusogeza huduma kwa wananchi kwa kujenga miundombinu inayoipa TAEC uwezo wa kutoa huduma kwa tija na ufanisi.

"Serikali imejenga majengo sita ya maabara na ofisi katika kanda tano yenye thamani ya takribani Sh. bilioni 28.11 ambapo majengo manne kati ya hayo, yamekamilika. Miradi hiyo ipo Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Mwanza na Zanzibar.

Aidha, Serikali ya Awamu Sita kupitia TAEC, ipo katika hatua za mwisho kukamalisha mpango wa ufadhili kwa vijana wa Kitanzania kusoma vyuo vya nje ya nchi masomo ya teknolojia na sayansi ya nyuklia katika ngazi ya shahada za uzamili.

Profesa Busagala alisema kila mwaka, vijana Watanzania watano hupata ufadhili huu lengo likiwa ni kuongeza idadi ya wataalam nchini katika nyanja ya teknolojia na sayansi ya nyuklia ili kuhakikisha kwamba nchi inanufaika ipasavyo na fursa za sayansi ya nyuklia.

Alisema serikali pia imewajengea uwezo wa kitaalam watumishi ili kujenga taifa lenye uwezo katika teknolojia ya nyuklia.


"Kwa kufuata mpango wa mafunzo uliowekwa na kuanza kutekelezwa, TAEC imeshasomesha watumishi 29 na inaendelea kusomesha wengine 32 ndani ya miaka mitatu. Jumla itakuwa watumishi 61. Hili ni muhimu sana kwa ustawi wa taifa letu katika sekta ya sayansi na teknolojia ya nyuklia," aliongeza Profesa Busagala.



# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO

## Stendi ya Mwenge inasubiri nini?



Kumekuwa na maelezo kwamba baada ya stendi mpya ya mabasi ya Mwenge kukamilika, mabasi yatapunguzwa kwenye Stendi ya Makumbusho ambayo kwa sasa imejaa na kuwa kama kichochoro.

Ukipita Stendi ya Mwenge ni kama kila kitu kiko tayari lakini bado haijaanza kutumika. Shida ni nini?




MAONI YA MHARIRI

# Waajiri boresheni maslahi, watumishi wajibikeni

LEO ni Mei Mosi ambayo ni siku maalumu kwa wafanyakazi kote duniani. Hapa nyumbani Tanzania, maadhimishio ya kitaifa yanafanyika jijini Arusha na mgeni rasmi anatazamiwa kuwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Jana viongozi mbalimbali wa kitaifa waliwasili Arusha kwa ajili ya kushiriki maadhimisho haya ikiwa ni pamoja, Makamu wa Rais Dkt. Phillip Mpango, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Dkt. Tulia Ackson.

Hakuna ubishi kwamba macho na masikio ya wafanyakazi nchini, leo yameelekezwa kwa Rais Dk. Samia kusikiliza atakavyoijibu kaulimbiu ya mwaka huu ya Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi nchini (Tucta) inayosema "Nyongeza ya mishahara, ni msingi wa mafao bora na kinga dhidi ya hali ngumu ya maisha."

Katika maadhimisho haya ambayo hufanyika takribani kila mkoa nchini mwetu, wafanyakazi ambao watakuwa wametekeleza majukumu yao vizuri wanatazamiwa kutunukiwa zawadi mbalimbali.

Ni vyema utamaduni huu wa kuwazawadia wafanyakazi wanaoonesha uwajibikaji mzuri na nidhamu kazini wakawa wanatambuliwa na kuzawadia ili kuwahamasisha kuwajibika zaidi na kuhamasisha wengine kufuata nyayo zao.

Mara nyingi, serikali ambayo ndio mwajiri mkuu, huwa inaongeza mishahara ya watumishi katika sekta ya umma pamoja ahadi nyingine za kuboresha maslahi ya wafanyakazi.

Kimsingi, serikali inapopandisha mshahara katika sekta ya umma, hali hiyo pia huathiri sekta binafsi kwa maana ya kwamba waajiri binafsi nao 'huzolewa' na upepo huo na kupandisha mishahara.

Wakati tungetamani kuona wafanyakazi wa Tanzania wakiongozewa mshahara, lakini ni vyema ijulikane pia kwamba serikali haitakuwa na uwezo wa kuongeza mishahara kama wafanyakazi hawahawa hawatakuwa wamezalisha kwa tija au kutoa huduma zilizotukuka katika kusaidia sekta nyingine ili kutunisha mfuko wa serikali.

Ndio maana Waswahili wanasema haki ya watumishi wa umma kuongezewa mshahara ili kuboresha maisha yao, ni lazima pia iende sambamba na kutimiza wajibu wao.

Hivyo, wafanyakazi wa Tanzania wanapaswa kutimiza wajibu wao wa kufanyakazi kwa uaminifu na kwa bidii ili kutengeneza mazingira ya nchi kuwa na uchumi mzuri utakaopelekea wafanyakazi hawa kulipwa mishahara minono zaidi.

Yote kwa yote ni imani yetu kwamba serikali na waajiri wengine watajitafakari katika kuhakikisha wanaboresha maslahi ya watumishi, lakini pia watumishi watumie maadhimisho haya kutafakari kama wanatumiza ipasavyo wajibu wao.

## Wasiliana nasi


**Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000

**Mhariri wa Habari:** +255768411003

**Mhariri Michezo:** +255784122020

**Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825

**S. L. P:** 15110, Dar es Salaam

**Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro

**Jengo la:** Aura Mall

**Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532

**Email:** uelekeohabari@gmail.com


## JICHO LANGU

# Anzisheni vyanzo vya mapato, punguzeni tozo

JANA kwenye kipindi cha maswali na majibu Bungeni, serikali ilipiga marufuku halmashauri zote nchini kuacha kutoza kodi kwenye mazao ya wakulima wa kawaida wanaosafirisha mazao yao kutoka shambani.

Kauli hiyo ilitolewa na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Jimbo la Bukene, Selemani Zedi aliyeitaka Serikali kutoa katazo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Nzega Vijijini kuwatoza kodi ya mazao ya wakulima wa kawaida katika halmashauri hiyo.

Kwanza ninampongeza Naibu Waziri kwa hatua hiyo huku nikikumbuka hivi karibuni kuona klipu ya mwanamama mmoja, mchuuzi wa kusafirisha vitunguu akilalamikia kitu kama hicho, kama sikosei ilikuwa mikoa ya kaskazini.

Mwanamama huyo alidai kwamba wamekuwa wakisumbuliwa sana na maofisa wa serikali za mitaa kusimamisha magari yanayotoa magunia ya bidhaa zao kutoka mashambani kwa wakulina na kuwadai ushuru na hongo kwa kusafirisha mazao yasiyofikia hata tani moja.

Yule mwanamke akakumbusha kwamba wakati wa Utawala wa Rais John Magufuli alipiga marufuku kwa wakurugenzi na watendaji wa halmashauri kuwatoza ushuru wasafirishaji wa mazao chini ya tani moja.

Akasema ingawa hajawahi kusikia kama kauli hiyo imetengeuliwa, wamekuwa wakitozwa na kupata usumbufu mkubwa.

Kilichonihamasisha kuandika ninayoyaandika ni kile ambacho serikali imekuwa ikizihamasisha halmashauri zetu kufanya, yaani kuondoa 'mentality' ya kutoza, kutoza, kutoza na badala yake ijikite zaidi katika kuanzisha miradi ya kuiingizia fedha na pia kupunguza kutegemea ruzuku ya serikali.

Ni katika muktadha huo, Waziri wa Tamisemi, Mohamed Mchengerwa anasema kigezo cha ziada cha kuzipima halmashauri zote nchini kwa sasa ni namna zitakavyobuni vyanzo vipya vya mapato kuanzia viwili na kuendelea kwa kila mwaka wa fedha.

> **kigezo cha ziada cha kuzipima halmashauri zote nchini kwa sasa ni namna zitakavyobuni vyanzo vipya vya mapato kuanzia viwili na kuendelea kwa kila mwaka wa fedha.**

Mchengerwa aliyasema hayo hivi karibuni wakati wa kufungua Mkutano wa 38 wa Jumuiya ya Serikali za Mitaa (ALAT) Taifa unaofanyika Zanzibar.

Alisema nguvu ya kila halmashauri ni mapato na ili iweze kutekeleza miradi yenye tija lazima kuwe na mapato ya uhakika.

Alisema kumekuwa na tabia ya halmashauri kuweka makadirio ya bajeti kidogo na kukusanya zaidi na kisha 'kujimwambafai' kwamba wamevuka malengo, jambo ambalo hata mimi ninaona halina maana!

Lakini Waziri akasisitiza kwamba ni vyema takwimu za bajeti za halmashauri ziendane na uhalisia wa tathmini ya vyanzo vya mapato.

Ni vyema sana halmashauri zianzishe vyanzo vingi vya mapato, hatua ambayo pia itaongeza ajira badala ya halmashauri zetu kukalia kwenye kutoza, kutoza na kutoza. Wajue zile wanazotoza ni huduma na anayeumia ni mwananchi wa kawaida anayelipia tozo hizo!

# Je; kuna ukweli wowote kuku wa `kizungu' wana madhara kiafya?



UPO uvumi mwingi kwamba nyama ya kuku wa kisasa maarufu kama kuku wa kizungu husababisha matatizo mengi ya afya.Je, kuku wa kizungu ni yupi, hukuzwa kwa njia gani na je; kuna hatari yoyote kwa miili ya binadamu wanapokula nyama ya kuku hawa?

Maelezo kutoka kwa wataalam:

**Kuku wa kizungu ni yupi?**

Kuku wa kizungu hufugwa kwenye mashamba. Hukua kwa muda mfupi sana. Mpango huu ulianzishwa kwa mara ya kwanza miaka ya 1930 katika nchi nyingi ikiwemo Marekani.

Mwishoni mwa miaka ya 1960, kuku wa nyama walienea ulimwenguni kote. Uzalishaji wa kuku hao uliongezeka kutokana na uhaba wa nyama ya kuku.

Nyama hii ya kuku, ni muhimu hasa kwa nchi nyingi ambako kuna uhaba wa protini.

Kipindi cha kukua, gharama ya chini na protini ya juu ni sababu kuu za ongezeko la mahitaji ya nyama hii.

Muthuramalingam, ambaye ana uzoefu wa muda mrefu katika usimamizi wa ufugaji wa kuku, anasema kuwa ufugaji wa kuku wa nyama, ulianza nchini India miaka ya 1970 na ulaji wa nyama uliongezeka sana kati ya mwaka 1980 na 1985.

Anasema katika kipindi cha miaka 30 tangu wakati huo, kuku wa nyama wamekuwa wengi kuliko kuku wa asili na sasa wanapatikana katika kila mkoa.

Kwa mujibu wa Tume ya Kudhibiti Wafugaji wa Kuku, wale wanaofugwa kwa muda mrefu kwa mayai, hujulikana kama 'layers' na wanaouzwa kwa nyama kwa muda mfupi, huitwa 'broilers'.

Kuku wa kizungu ni aina maalum ya kuku wa Cornish. Aina hii ya kuku ina uwezo wa kukua haraka sana. Tangu mwaka 1970, wameanza kufuga kuku wa aina hii kwa ajili ya nyama," alisema daktari wa watoto na mshauri wa lishe Dk. Arun Kumar.

"Kutokana na mabadiliko ya kisasa katika tasnia hii, kuku wa nyama ambao walikuwa wakikua kwa siku 60, sasa wanakua ndani ya siku 32. Sababu yake ni mabadiliko ya chakula kinachotolewa kwa ajili ya kuku hawa," anasema.





**Kuna tofauti gani kati ya kuku wa kizungu na wa kienyeji?**

Kwa kawaida, huchukua miezi sita au zaidi kukuza kuku wa kienyeji. Lakini, kuku wa nyama hupata uzito wa zaidi ya kilo mbili ndani ya siku 35 hadi siku 45.

Hata hivyo, kuku wa kizungu hawana kinga sawa na kuku wa kienyeji. Kwa hiyo, kuku wa nyama wanahitaji kuchanjwa mara kadhaa.

Mtaalamu wa lishe, Meenakshi Bajaj, anasema kuna miongozo maalum ya ufugaji wa kuku wa nyama.

Tume ya Kudhibiti Wafugaji wa Kuku, imetoa mwongozo wa jinsi ya ufugaji wa kuku wa nyama unaostahili kufanywa.

Kwa mujibu wa miongozo hii, kuku wa kizungu wanapaswa kufugwa kwa muda wa kati ya wiki sita na nane.

Miongozo imeamuliwa kuhusu aina gani ya chakula, maji, mazingira ya kulea, chanjo na dawa wanapewa.

Tume ya Kudhibiti Ufugaji wa Kuku, inapendekeza ufugaji wa kuku wa kizungu kwa njia yenye afya.

Ripoti nyingi zinadai kuwa kuku wa kizungu hudungwa sindano za homoni kuwafanya wakue haraka.

Taarifa hizi zinasema kuwa wale wanaokula hupata matatizo yanayohusiana na homoni na vifaranga hubalehe mapema.

**Je, ni kweli kuku hawa wanadungwa sindano za homoni?**

Muthuramalingam anasema kuwa jambo kama hilo halitafanyika.

"Kuku hawa wanapokea, hushambuliwa na virusi vya aina mbalimbali, sawa na binadamu anavyochanjwa dhidi ya virusi, kuku hawa pia huchanjwa, mbali na hayo hakuna dawa nyingine,"

>> INAENDELEA UK. 8

> **Tume ya Kudhibiti Wafugaji wa Kuku, imetoa mwongozo wa jinsi ya ufugaji wa kuku wa nyama unaostahili kufanywa. Kwa mujibu wa miongozo hii, kuku wa kizungu wanapaswa kufugwa kwa muda wa kati ya wiki sita na nane.**

# Je; kuna ukweli wowote kuku wa `kizungu' wana madhara kiafya?



>> INATOKA UK. 7

anasema.

Naibu Katibu wa Kamati ya Udhibiti wa Wafugaji wa Kuku, Sarath anasema kuwa ikiwa homoni itawekwa kwa kila kuku, gharama itaongezeka sana.

Hakutakuwa na fursa kama hiyo. Ikiwa kitu kitatokea kwa kuku hawa, antibiotics itatolewa, anasema.

Kuku wa nyama hukua ndani ya siku 42 hadi 45. Hawapewi homoni. "Hawa sio kama wanyama wengine wakubwa," anafafanua.

'Hakuna kitu kama homoni ya ukuaji'

"Watu wengi wanadhani kuku hawa wanafugwa kwa homoni za ukuaji. Lakini hakuna homoni kama hiyo. Homoni hutumika kwa watoto waliodumaa ili kuongeza urefu wao.

Iwapo zitatumika kwa kuku, wanastahili wapewe nne kila siku kwa siku 40. Hiyo ina maana kwamba gharama itakuwa ya juu.

"Ili kuwakinga kuku hawa dhidi ya maambukizi ya virusi, chanjo tano hutolewa kwa kila kuku. Wengi huzichukulia kama sindano za homoni," anasema.

Meenakshi, mtaalamu wa lishe, anasema kwa hakika kuna hatari katika kufuga kuku katika mashamba ya kuku bila kufuata sheria zilizowekwa na Tume ya Kudhibiti Wafugaji wa Kuku.

Aidha, Profesa wa Chuo cha Madaktari cha Serikali cha Chennai, Stanley na Mkuu wa Idara ya Matibabu, S Chandrasekhar, pia anatoa maoni sawa wakati watu wanakula aina ya kuku ambao wamepewa kemikali na antibiotics.

"Maelfu ya kuku wanafugwa kwenye viwanda vya kuku kwa kuongeza kemikali kwa kuku hao kwa ajili ya nyama ya ziada.




Viua sumu vilivyo na nguvu, huwekwa kwenye vyakula vyao ili kuzuia virusi vya aina yoyote kuwashambulia. Kemikali hizi huitwa visumbufu vya endocrine.

Anasema ulaji wa vitu vyenye kemikali hizo, unaweza kusababisha matatizo ya kiafya mfano ugumba, uvimbe kwenye tezi dume na kukoma hedhi mapema.

Chandrasekhar anasema kuwa kemikali katika kuku wa nyama, si sababu pekee ya magonjwa haya, lakini hii inaweza pia kuwa moja ya sababu.

Dk. Arun Kumar, anasema kula kuku wa nyama, hakuleti hatari yoyote kwa watu

Dk Kumar anasema licha ya kuenea kwa matumizi ya antibiotics katika ufugaji wa kuku wa kizungu, haziathiri watu moja kwa moja.

"Mara nyingi watu hupewa dawa za kuua viua sumu, hivyo vinavyopewa kuku.

Dk.Kumar anasema kuwa kula kuku wa nyama hakuleti hatari kwa wanadamu.

"Kuku wa nyama ni nyeti sana, hutolewa kwa dozi ndogo kuliko inavyotakiwa, dawa hizi za antibiotics hutolewa kwa maelekezo ya daktari wa mifugo. Hakuna nafasi ya kushambulia binadamu, kisayansi hili haliwezekani," anasisitiza.

### Walaji wa biryani wanapaswa kufanya nini?

Uchunguzi wa hivi karibuni umebaini kuwa biryani ilikuwa chakula nambari moja kilichoagizwa na kampuni za utoaji wa chakula nchini India mwaka jana.

Kuku biryani, ni maarufu sana kwa Wahindi. Kula kuku kupita kiasi pia ni hatari. Lakini, mtaalamu wa lishe, Meenakshi anasema kwamba hatari hizi zinaweza kuepukwa.

"Unaweza kula gramu 100 za kuku mara tatu kwa wiki. Mbali na kukaanga, inaweza kuliwa katika mchuzi au kuchemshwa. Katika kesi ya biryani, kula mara mbili kwa mwezi kwa kiasi," anasema. BBC.





Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo

JARIDA

Jungu Kuu

| Jumatano Mei 1-7, 2024 |

JAMII UCHUMI SIASA

Jarida hili haliuzwi


# Mei Mosi 1995 Nyerere alitaka kiongozi kaliba ya Samia



UK. 12 & 13

# Wafanyakazi wa majumbani wasiendelee kusahaulika

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYAKAZI wa majumbani ni kundi kubwa ambalo si vyema kupuuzwa katika karne hii. Wafanyakazi hawa wana mchango mkubwa, si kwa familia tu zilizowaajiri bali pia kwa taifa zima la Tanzania.

Wakati fulani, takwimu za Shirika la Kazi Duniani (ILO) zilionesha kuwa wafanyakazi wa majumbani milioni 5.2 wameajiriwa kwenye sekta hii katika bara la Afrika pekee. Hii ni takwimu ya mwaka 2008, hivyo idadi ni zaidi ya hiyo kwa mwaka huu wa 2024.

Wafanyakazi wa majumbani wana mchango mkubwa kwa familia na kwa pato la nchi, japo suala hili halionekani kirahisi kwa jamii. Kufanya kazi majumbani, huwapa fursa wafanyakazi wengine kufanya kazi za uzalishaji katika sekta rasmi na sekta isiyo rasmi kwa ufanisi. Hivyo bila wao utendaji wa watumishi hawa unakuwa mashakani.

Kwa mujibu wa Chama cha Wafanyakazi wa Hifadhi, Mahoteli, Majumbani, Huduma za Jamii na Ushauri (CHODAWU) mfanyakazi wa majumbani ni mtu yoyote anayehusika na kazi za majumbani katika mahusiano ya ajira.

Chama hiki kimezianisha kazi za majumbani kuwa ni "kazi zinazofanyika ndani au kwa ajili ya kaya moja au zaidi". Chama kilizitaja kazi hizi kuwa ni usafi wa nyumba, upishi, kufua na kupiga pasi, kulea watoto, wazee na wagonjwa katika familia, kuangalia bustani, ulinzi wa nyumba na udereva wa gari la familia na kutunza wanyama katika kaya.

Chama hicho kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO) na wadau wengine wamekuwa wakiitaka serikali iridhie mkataba namba 189 wa kazi zenye staha kwa wafanyakazi wa majumbani, sheria za kazi na kusisitiza mazingira bora ya kazi kwa wafanyakazi wa majumbani.

Umoja wa Mataifa kupitia Shirika la Kazi Duniani (ILO) katika Mkutano wake wa 100 uliofanyika Juni, 2011 Jijini Geneva, Switzerland ulipitisha mkataba wa kimataifa namba 189 pamoja na mapendekezo yake namba 201.

Katika mkataba huo wa kimataifa iliazimiwa kuwa wafanyakazi wa majumbani wapewe kazi za heshima kama wafanyakazi wengine katika sekta zingine na wasitengwe katika mifuko ya hifadhi ya jamii.

Serikali ya Tanzania iliunga mkono mkataba huu hivyo sasa ni vyema kwa serikali yetu kuridhia ili mkataba huu uweze kutumika katika sheria zetu za nchi.

Mkataba huu utakaporidhiwa utakomesha manyanyaso na dhuluma wanazofanyiwa wafanyakazi hawa kama vile wengine kutolipwa ujira kwa kisingizio cha udugu. Wengine wanafanya kazi mishahara inatumwa makwao ama kwa mawakala waliowaunganisha kwenye ajira hizo.

Wengine wamekuwa wakifanya kazi kwa ujira wa lishe na malazi tu. Wengi miongoni mwao wanafanyishwa kazi zaidi ya muda wa masaa ya kazi yaliyowekwa kisheria. Hawapewi fursa za kujiendeleza kielimu ama kiujuzi. Likizo ikiwa ni sehemu ya haki katika ajira, lakini wengi wao hawazipati na wanahofu hata kuhoji kwa kuogopa kupoteza vibarua vyao.

Endapo utafanyika utafiti wa jinsi gani wafanyakazi wa majumbani huchangia katika uchumi wa Taifa matokeo yatakuwa ya ajabu.

Wafanyakazi wa majumbani kama wafanyakazi wengine wana haki zifuatazo: Kulipwa mishahara ama ujira wa kazi wanazofanya. Wafanyakazi hawa wana muda wa kazi na muda wa kupumzika kama zilivyo kazi zingine. Muda wa kazi kwa mujibu wa sheria za nchi ni saa tisa.

Mbali na muda wa mapumziko ya kila siku pia kuna mapumziko ya kila wiki. Halikadhalika kuna muda kwa ajili ya shughuli binafsi ziwe za kujiendeleza kwa ajili ya ustawi wake ama faragha.

Wafanyakazi hawa haki ya kupewa likizo zote kuanzia, likizo ya mwaka na malipo yake, likizo ya uzazi pindi inapotokea suala la uzazi, likizo ya ugonjwa na likizo ya huruma.

Pia wana haki ya kupata matibabu, kufanya kazi katika mazingira ya afya na usalama na kutetewa haki zao kupitia vyombo vya sheria.

Wana haki pia ya kujiunga na vyama vya wafanyakazi kama vile Chodawu, wanahaki ya kujiunga na mifuko ya hifadhi ya jamii kama vile NSSF, LAPF na PPF ili kujiwekea akiba.



Mbali ya kuwa na haki ya kufanya kazi zenye staha lakini pia wana haki ya kufanya majadiliano na waajiri ama vyama vya waajiri kwa lengo la kuboresha haki na maslahi bora ya kazi.

Suala la umri katika ajira za majumbani limekua ni tatizo lingine kwani watoto wamekuwa wakifanyishwa kazi hizi kinyume na utaratibu. Imekuwa ni rahisi watoto kupatikana na kutumikishwa kwenye ajira hizi. Umri unaostahili kufanya kazi za majumbani ni miaka 18 na kuendelea.

Wenye umri chini ya miaka 18 lakini si chini ya 15 wanaweza kuajiriwa kuwa wafanyakazi wa majumbani lakini kazi zao zisiwanyime elimu ya lazima, mafunzo ya ufundi ama kijiendeleza zaidi. Wale wanaoishi na waajiri inatakiwa wapewe maisha yenye staha na waajiri waheshimu faragha ya wafanyakazi hao.

Ikumbiukwe kwamba Tanzani ni miongoni mwa nchi za kwanza kusaini Mkataba wa Kimataifa wa Wafanyakazi za Majumbani.

Sasa kinachohitajika ni serikali kuridhia mkataba huu kuwa sheria ili utekelezaji wake uweze kuwakomboa wafanyakazi hawa na waondokane na adhaa zinazowakabili.

Baadhi ya haki za wafanyakazi wa majumbani kama zilivyoorodheshwa, kwa wetu wengine, kutokana na mazoea wanaweza kushangaa na kujiuliza, "Yaani hausigeli nimpe likizo ya malipo, nimpe muda wa mapumziko kila siku."

Mawazo kama hayo yanatokana mazoea na mitazamo ya kikale, lakini utaratibu ukibadilika haitachukua muda mrefu watu watazoea. Na mfanyakazi wa ndani akitendewa hayo, kinadharia atafanya kazi vizuri zaidi na upatikanaji wa wafanyakazi hawa utakuwa mwepesi.

Katika kubadilisha mitazamo ya hovyo, Chadawu imekuwa ikihimiza wafanyakazi majumbani wasiitwe dada au beki namba tatu bali "mfanyakazi wa nyumbani."

Hivyo, tutumie Mei Dei kuisukuma serikali kuridhia mkataba huo.

Hamisi Kibari

TUKUBALIANE KUTOKUBALIANA

Simu: 0758143457

# Mei Mosi ichochee uwajibikaji

LEO ni Mei Mosi na kama kawaida, Watanzania, hususani wafanyakazi, wanaungana na wenzao duniani kote kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani.

Ni siku ambayo wafanyakazi duniani kote hukaa chini kutathmini maendeleo yao, matatizo yao na kuyaweka wazi kwa waajiri wao.

Siku hii huwa na uzito mkubwa kwa wafanyakazi kutokana na maadhmisho yake katika nchi mbalimbali kuhutubiwa na viongozi mashuhuri wa nchi ambao pia ni waajiri wakubwa.

Kwa upande wa Tanzania, sherehe za Mei Mosi zitafanyika pale mkoani Arusha, na mgeni rasmi si mwingine bali Rais Samia Suluhu Hassan ambaye atawahutubia wafanyakazi na bila shaka atazingumzia maslahi yao.

Mei Mosi imekuwa ikiadhimishwa kwa hisia tofauti na wafanyakazi huku wakibeba mabango yenye jumbe mbalimbali kwa waajiri wao, ikiwa ni pamoja na kufikisha kilio chao au hata matarajio yao.

Mei Mosi ya mwaka huu, kama zilivyo nyingine bila shaka itaambatana na neema kwa baadhi ya wafanyakazi waliofanyakazi zao kwa bidii, nidhamu na ufanisi na hivyo kutunukiwa zawadi ya kuwa wafanyakazi bora.

Pamoja na yote zikiwemo salamu mbalimbali, ugawaji wa zawadi kwa wafanyakazi bora na mengine mengi yanayofanyika, ukweli ni kwamba shauku kubwa ya wafanyakazi huwa ni kusikia serikali ikitangaza nyongeza za mishara.

Lakini ambacho wafanyakazi wanapaswa kuzingatia ni kwamba mshahara hautoki hewani, bali ni kutokana na uwezo wa serikali kutegemea maendeleo ya uzalishaji na utoaji huduma bora katika nchi yetu.

Kwa maana hiyo, kadri wafanyakazi, iwe wa sekta binafsi au ya umma watakavyochapa kazi zaidi, wakazalisha zaidi, wakauza bidhaa zaidi au kutoa huduma bora zaidi, uchumi utapanda zaidi na maokoto yataongezeka maradufu. Kwa maana hiyo serikali kuongeza mishahara itakuwa sawa na kumsukuma mlevi.

Kimsingi, serikali inapopandisha mshahara katika sekta ya umma, hali hiyo pia huathiri sekta binafsi kwa maana ya kwamba waajiri binafsi nao 'huzolewa' na upepo huo na kupandisha mishahara.

Kimsingi huwa ni azma ya serikali kuona kuwa kila mfanyakazi anapata mshahara unaokidhi gharama ya maisha kwa sasa, ila changamoto, kama ambavyo nimeeleza hapo juu kitu ambacho limekuwa kikigomba ni uwezo mdogo wa serikali kifedha.

Katika mazingira kama hayo serikali inashindwa kuongeza kiwango kikubwa cha mshahara kwa mara moja, lakini imekuwa ikifanya hivyo kwa awamu.

Hata hivyo, ninachosema hapa ni kwamba wafanyakazi wetu wakiamua kuchapa kazi kama siafu au zaidi ya ambavyo tunasika wenzetu Wachina wanavyoshambulia kazi, suala la mishahara kuongezeka litakuwa mikononi mwao.

Kimsingi, jukumu la mfanyakazi makini ni kufanya kazi kwa bidii na nidhamu kubwa ili kuongeza ufanisi na kudhihirisha kwamba ni kweli ana haki ya kupandishwa mshahara kwani Waswahili wanasema hakuna haki bila wajibu.

Hivyo, wafanyakazi wa Tanzania wanapaswa kutimiza wajibu wao wa kufanyakazi kwa uaminifu na kwa bidii ili kutengeneza mazingira ya nchi kuwa na uchumi mzuri utakaopelekea wafanyakazi hawa kulipwa mishahara minono zaidi.

Hivi karibuni, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dkt. Dotto Biteko aliwataka wafanyakazi wa Shirika la Umeme (Tanesco) kuhakikisha suala la mteja linalowezekana leo lisingoje kesho.

Hebu fikiria katika mazingira ambayo mteja wa Tanesco, tuseme mfanyabishara au mwekezaji, anatoa taarifa ya kuhitaji umeme, au kutokea hitilafu kwenye eneo lake halafu wahusika wanaanza kumzungusha kwa uzembe au kujenga mazingira ya kuomba rushwa kiasi kwamba jambo la kufanywa siku moja linachukua wiki mbili. Hapo Tanesco itakuwa imepoteza shilingi ngapi za kulipwa matumizi ya umeme na huyu mteja? Kama ni mlipa kodi au ushuru, serikali itakiwa imepoteza kiasi gani cha fedha?

Wakati umefika sasa kwa wafanyakazi kuacha tabia ya kulilia maslahi makubwa huku wakishindwa kutimiza wajibu wao kwa maana ya kuwa waadilifu kazini kwa kuutumikia umma kadri ya uwezo wao na kuwa kifua mbele kwamba kuna kitu kizuri wameifanyia nchi yao.

Nirudie tena kusema kwamba uungwana ni kabla ya mtu hajadai haki zaidi na marupurupu, anapaswa kwanza kutekeleza wajibu.

Kubwa ambalo wafanyakazi wa Tanzania wanapaswa kujiepusha nalo ni kujihusisha na vitendo vya ufisadi na rushwa ambavyo vinadidimiza uchumi wa nchi na kunyima haki za wananchi.

Baadhi ya wafanyakazi, hususani katika sekta ya umma, wamekuwa na mazoea ya kutowajibika vizuri mahala pao pa kazi ikiwmo kutumia muda mwingi kufanya shughuli nyingine zisizohusiana na ofisi au idara waliopo au kukalia kupiga 'stori' badala ya kuchapa kazi.



Si jambo la kushangaza kwenda kwenye ofisi fulani na ukaambiwa msubiri ofisa amekwenda kunywa chai na ukatumia hata saa mbili ukisubiri huduma kwa ofisa huyo wa umma anayekunywa chai.

Hili ni jambo la aibu, na kila mmoja atambue kuwa kwa kufanya hivyo siokwamba anaathiri taifa tu, bali pia anajiathiri yeye mwenyewe kama mfanyakazi, kwani mwisho wa siku serikali itashindwa kufikia malengo yake kiuchumi kutokana na uzalishaji kuwa mdogo.

Mtoa huduma anapomkwamisha mtu kwa saa mbili ina maana kwamba wote wawili katika muda huo watakuwa hawazilishi na hivyo kurudisha maendeleo ya nchi nyuma.

Uchumi wa taifa hili hautakuzwa na watu wa nje isipokuwa ni Watanzania wenyewe, na hakuna njia nyingine ya kukuza uchumi ila ni kwa kuweka nidhamu na kufanyakazi kwa bidii na uaminifu. Ni wakati sasa wa kuondoa dhana iliyojengeka kwamba Watanzania ni wavivu na wanaopenda visingizio mahala pa kazi.

Hakika kila mmoja wetu akitimizwa wajibu wake ipasavyo hakuna shaka kwamba kizazi cha sasa na kijacho, yaani watoto wa wafanyakazi walioko maofisini sasa watafaida matunda ya nchi yao, ikiwemo kupokea mishahara minono na marupurupu mengine.

Nchi zilizopiga hatua za maendeleo ambazo leo tunawaona kama wabwana wakubwa wakiwa na uchumi mzuri, kikubwa baada ya kuwekeza kwenye elimu, walijifunza nidhamu na uwajibikaji, jambo ambalo hata Watanzania tunaliweza tukiamua kwa dhati.



# Mei Mosi 1995 Nyerere alitaka kiongozi kaliba ya Samia

**Na Hamid Yassin**

LEO ni Siku ya Wafanyakazi Duniani, maarufu kama Mei Mosi. Unaweza kuiadhimisha vile upendavyo hata kama si mfanyakazi. Mimi kwa upande wangu nimeamua kuienzi siku hii kwa kukumbuka hotuba ya mwisho ya Baba wa Taifa hili, hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kabla ya uchaguzi mkuu wa kwanza chini ya mfumo wa vyama vingi ya siasa mwaka 1995.

Sasa unaelekea mwaka wa 25 tangu Watanzania tumpoteze Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, mwasisi wa Taifa letu la Tanzania aliyeaga dunia Oktoba 14, 1999 katika Hospitali ya Mt. Thomas iliyopo London, Uingereza.

Katika kipindi chote hicho Watanzania tunaendelea kumkumbuka kwa maono aliyokuwa nayo juu ya nchi yetu lakini pia uhitaji wa kiongozi mzalendo, mwadilifu na mwenye utayari wa kuleta maendeleo kwa watu wake ili kukidhi matarajio yao.

## HOTUBA YA MEI MOSI 1995

Tukiwa tunaingia miaka ya uchaguzi, yaani huu wa 2024 ambao mwezi Oktoba tutakuwa na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na ule wa mwakani 2025 tutapokuwa na Uchaguzi Mkuu wa Taifa, hotuba aliyotoa Mwalimu Nyerere kule Mbeya mwaka 1995 kwenye sherehe za Mei Mosi imenijia kichwani mwangu!

Siyo siri, miongoni mwa hotuba zake maarufu ni ile aliyoitoa mkoani Mbeya katika kilele cha Mei Mosi, mwaka 1995 kwenye Uwanja wa Sokoine.

Hotuba ile ilikuwa ni hotuba yake ya mwisho kabla ya kufanyika kwa mara ya kwanza Uchaguzi Mkuu katika mfumo wa vyama vingi vya kisiasa nchini baadaye mwaka huo 1995.

Pamoja na kwamba Mwalimu alizungumzia masuala ya wafanyakazi, maendeleo na kukemea dosari zilizoanza kujitokeza nchini, kwa hisia pia alisisitiza wajibu wa viongozi watakaochaguliwa kuanzia ngazi ya diwani, mbunge hadi rais katika kutatua matatizo ya jamii zao.

## NYERERE NA NDOTO YA RAIS

Katika hotuba hiyo alisema, "Tunataka mtu anayetaka kuwa rais wetu ajiulize anataka kuifanyia nini nchi yetu na sio nchi yetu itamfanyia nini?"

Hili swali linalomtaka kila anayetaka kuwa mgombea wa chama chochote na katika ngazi yoyote kujiuliza kwa dhati kabisa. Anataka kuidiaje nchi yetu, amepanga kuwapa nini wsnanchi ambacho watakikumbuka dahari.

Aidha, Mwalimu alitanabahisha kuwa mgombea atakayechaguliwa akerwe na hali ya umasikini wa Watanzania na kwamba kero hiyo imsukume kuwa tayari kuishughulikia iwe ni katika ngazi ya udiwani, ubunge na urais.

Vilevile, alionya wagombea kuwa Ikulu si mahali pa kukimbilia isipokuwa ni mahali ambapo unakutana na matatizo mengi ya wananchi kama vile njaa, umaskini na huna budi





kuyatatua matatizo hayo kwa manufaa ya taifa zima.

"Ukiona mtu anapakimbilia, na hasa anapotumia vipesa kwenda Ikulu, mtu huyo ni wa kuogopa kama ukoma!...... Mtanzania wa leo hawezi kununua watu bila kwanza yeye kununuliwa, na kama kanunuliwa atazilipaje, ... kama kakopa atazirudishaje?" Alihoji Mwalimu.

**VIONGOZI WAFIA NCHI**

Tunapoelekea katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu na ule Mkuu Oktoba mwakani 2025, nakumbuka namna Mwalimu Nyerere alivyoipenda nchi yake, alijitoa kwa nadharia na vitendo, alikuwa mshauri katika masuala mbalimbali kuanzia siasa, uchumi, na hata masuala ya kijamii.

Mwalimu aliipenda nchi yake na alikuwa tayari kusaidiana na viongozi wengine wanaoijenga nchi bila kujali itikadi za kisiasa au kidini.

Alikuwa kiongozi mkweli asiyetetereka kwani alikuwa tayari kuwapinga na kuwakemea bila woga viongozi wanaoharibu nchi hata kama wanatoka katika chama chake.

Alitamani kuona taifa linaongozwa na kiongozi mwadilifu, jasiri na shujaa, kiongozi mwenye nia ya dhati ya kupambana na maadui ujinga, maradhi na njaa ili kuleta maendeleo ya kiuchumi kwa watu.

**SAMIA NA NDOTO ZA NYERERE**

Kupitia hotuba zake, ni kama vile Baba wa Taifa aliota ndoto juu ya Rais wa Awamu ya Sita, Dk. Samia Suluhu Hassani. Miaka mitatu iliyopita Watanzania tulishuhudia Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikitupatia Rais huyu kufuatia kifo cha ghafla cha mtangulizi wake, Dk. John Pombe Magufuli.

Nasema Katiba ilitupatia Dk. Samia, hatukumchagua sisi raia kwa njia ya sanduku la kura ili aiongoze nchi yetu kwa kipindi cha miaka hii inayokaribia minne na baadaye Mwenyezi Mungu ikimpendeza Inshallah aingie tena madarakani hapo mwakani kwa ridhaa ya wananchi.

Katika uchaguzi wa mwaka 2020, uliohusisha na kushindanisha wagombea toka vyama tofauti, mgombea wa urais wa Chama tawala nchini, CCM, hayati Magufuli, alitangazwa kuibuka mshindi wa kiti cha urais sambamba na aliyekuwa mgombea mwenza Dk. Samia.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), chini ya Mwenyekiti wa Tume hiyo wakati huo, Jaji Mstaafu Simistokles Kaijage ilimtangaza rasmi John Pombe Magufuli kuwa ndiye rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwamba alishinda kwa kupata kura 12,516,252 sawa na asilimia 84 za kura zote zilizopigwa dhidi ya mshindani wake wa karibu, Tundu Lissu aliyepata kura 1, 933, 271 sawa na asilimia 13 ya kura zote zilizopigwa.

Watanzania walimpenda sana hayati Magufuli, lakini Mwenyezi Mungu alimpenda zaidi, hivyo ilipofika Machi 17 mwaka 2021 alimchukua kiumbe wake na kama nilivyosema hapo juu kwa mujibu wa Katiba yetu mara moja Makamu wake, Dk. Samia aliapishwa Machi 19, 2021kushika wadhifa huo.

Tangu alipoapishwa rasmi, Machi 19 mwaka 2021, Rais Dk. Samia amedhihirisha kwa vitendo kuwa ile ndoto ya Baba wa Taifa katika hotuba yake ya Mei Mosi, 1995 sasa imetimia kwa kuwa amepatikana kiongozi anayeguswa na shida za wananchi kwa dhati ya moyo wake, sifa ambayo Baba wa Taifa alikuwa akisisitizia.

**HOTUBA YA SAMIA BUNGENI**

Katika hotuba yake ya kwanza aliyoitoa Bungeni Jijini Dodoma, Aprili 22 mwaka 2021, Dk. Samia alieleza azma na mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Sita ambao pamoja na kudumisha mazuri ya awamu zote zilizopita, lakini pia kuendeleza mema yaliyopo na kuleta mengine mapya.

Dk. Samia alisema jitihada zaidi zinahitajika katika kukuza uchumi na vilevile kupambana na umaskini, rushwa, ubadhirifu, urasimu, upotevu wa mapato, uzembe sehemu za kazi na migogoro ya wakulima na wafugaji.

Pia Dk. Samia alizungumzia maeneo mengine kama upungufu wa huduma muhimu za kijamii kama vile maji, nishati, afya, elimu, ajira na ubovu wa miundombinu, kwamba chini ya uongozi wake atayasimamia kikamilifu na sasa baada ya miaka hii michache mitatu kila Mtanzania ni shuhuda wa kasi kubwa ya kutimiza ahadi zake kikamilifu.

Aidha, Dk. Samia aliahidi kushughulikia matatizo ya wananchi bila kujali itikadi za vyama vya siasa isipokuwa kutanguliza nchi mbele kwa kuwa matarajio na matumaini ya wananchi katika kipindi cha uongozi wake ni makubwa.

"Wanachotaka kuona wananchi ni nchi yetu kupiga hatua kubwa za maendeleo zitakazojibu matumaini yao na kutatua shida na kero zao. Nyie na mimi baada ya hii miaka yangu ya awali tutapimwa kwa namna tutakavyokuwa tumetekeleza mambo ambayo tumewaahidi Watanzania wenzetu," alisema Rais Dk. Samia.

**SAMIA AUPIGA MWINGI KILA SEKTA**

Wakati tunaenzi mawazo na nasaha za Baba wa Taifa kuelekea miaka 25 tangu alipofariki, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mama imefanikiwa kuleta maendeleo kwa wananchi kwa kipindi kifupi.

Aidha, kama ilivyokuwa Awamu ya Tano, Awamu hii pia imeendelea kuimarisha nidhamu na uwajibikaji kwa watumishi wa umma, imeondoa urasimu, na hivyo kupunguza rushwa kwa kiasi kikubwa ndani ya Serikali, kupunguza sherehe na warsha na kuelekeza fedha zilizokuwa zitumike kwenye huduma za jamii.

Kwa upande wa kilimo, Serikali ya Awamu ya Sita, imeimarisha upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima huku ikifikia hatua ya kutoa ruzuku kwenye mbolea pale ilipopanda ikiwa ni pamoja na kuimarisha vyama vya ushirika ili kuwawezesha wakulima kuzalisha kwa tija.

Ili kuwashirikisha vijana kwenye kilimo cha kisasa serikali ya Dk. Samia imekuja na kitu kinachoitwa jenga kesho iliyo bora (BBT) huku ikiwa imeongoza maradufu maeneo ya skimu za umwagiliaji na huduma za ugani.

Kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kuanzia mwaka 2015 hadi mwezi, Aprili, 2021, vijiji 9,112 kati ya 12,268 ambavyo ni sawa na asilimia 80 vilikuwa vimepatiwa umeme, lakini sasa vijiji vingi vimefikiwa na umeme na sasa Serikali ya Awamu ya Sita mwaka huu 2024 imeanza mpango wa kufikisha umeme wa REA siyo vijijini tena, bali hadi vitongojini.

Aidha, sekta ya afya imeimarishwa ambapo upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na huduma za matibabu zimekuwa za uhakika ikiwa ni pamoja na kujenga na kukarabati vituo vya afya, hospitali za Wilaya, hospitali za rufaa na za kanda pamoja na kuongeza huduma za kibingwa ambazo hapo awali zilikuwa zinapatikana nje ya nchi.

Hatua nyingine zilizochukuliwa katika kuwaletea maendeleo wananchi wa kada mbalimbali ni pamoja na kuimarishwa kwa miundombinu, sekta ya usafiri na usafirishaji, uanzishwaji wa masoko ya madini na utoaji wa risiti za kielektroniki.

Ujenzi wa mradi mkubwa wa kufua umeme wa Bonde la Rufiji wenye uwezo wa kuzalisha megawati 2,115 unaoendelea kwa gharama ya shilingi trilioni 6.5, sasa vinu viwili vyenye uwezo wa kuzalisha umeme wa megawati 670 tayari vimewashwa na kuingizwa kwenye gridi ya taifa.

Ule ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) itakayogharimu shilingi trilioni 7 upo kwenye kasi ya kimbunga na juzi hapa treni ya majaribio iliwachukua viongozi wa dini wa madhehebu yote hadi Dodoma walipokwenda kuliombea taifa.

Aidha, viwanda zaidi ya 12,300 vikiwemo vidogo, vikubwa na vya kati vimeanzishwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Mafanikio haya yanatokana na ujasiri wa Rais Dk. Samia kufanya maamuzi magumu ambayo yalionekana hayawezekani machoni mwa wengi kutokana na yeye Rais kuwa ndiye kiongozi wa kwanza mwanamke wa ngazi ya juu kabisa ya taifa hili.

Julai mwaka 2020, Benki ya Dunia iliitangaza Tanzania kuwa miongoni mwa mataifa yenye uchumi wa kipato cha kati wa dola 1,006 hadi 3,995 kwa mwaka, katika hali ya kushangaza ghafla tulishuka kiuchumi na kuondolewa huko kwenye nchi zenye uchumi wa kati duniani, lakini juzi kwenye hotuba yake kwa taifa mkesha wa kuamkia Siku ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Rais Dk. Samia aliutangazia umma wa Watanzania kwamba tumerejea tena kwa kishindo kwenye uchumi wa kati.

Hali hii inayoelezwa kuwa imetokana na utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati iliyoweza kukuza ajira kwa wananchi na kuinua vipato vyao.

Tunapoendelea kuadhimisha miaka 60 ya Muungano na Mei Mosi ya mwaka huu, tunayo sababu ya kujivunia mafanikio yaliyopatikana sasa nchini kwa kuwa ndiyo ilikuwa ndoto ya Baba wa Taifa ya mwaka 1995.

Ndoto ya kuona Watanzania tunaishi kwa vitendo hasa tunapoangalia hatua kubwa za maendeleo ambazo nchi yetu imezipiga kwa muda huu mfupi wa miaka mitatu ya Dk. Samia. Ni hali halisi.

Hivyo, tunatarajia vyama vyote vya siasa kuanzia uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu na ule mkuu mwakani katika ngazi zote, vitasimamisha wagombea wenye sifa kama Dk. Samia Suluhu Hassan ili kuenzi yale aliyotamka Baba wa Taifa hili, hayati Mwalimu Nyerere kwenye Sherehe zile za Mei Mosi za mwaka 1995!

Alamsiki.

Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787 au 0784 122 020

# Unapolalamikia maisha magumu wewe binafsi umechangiaje?

**Na Dkt. Felician Kilahama**

Nianze sehemu ya pili ya makala hii kwa kutoa shukrani za dhati kwa Mungu aliye muumba wetu na mwingi wa kuturehemu na kututakia mema bila kuchoka, jina lake libarikiwe. Aamin.

Sehemu ya kwanza ya mfululizo wa makala haya nililiihitimisha kwa kuwashauri vijana wetu kwamba wawe wepesi wa kumtanguliza Mwenyezi Mungu aliye Alfa na Omega na wajue kuwa kwake hakuna kinachoshindikana.

Mungu akiwa upande wao hatowaacha waangamie kwa kukosa maarifa; bali atawawezesha kufanya shughuli zao kwa ungalifu na weledi mkubwa. Aliye na macho haambiwi tazama na mwenye masikio na asikie na kufanya uamuzi sahihi, kwa wakati.

Ushauri huo unalenga kujenga kizazi kinachomheshimu na kumpa Mungu Utukufu anaoustahili kama muumbaji wetu na aliye asili ya mema yote.

Kimsingi, na kwa uzoefu tulionao; hakuna binadamu aliyejinyenyekeza mbele ya Mungu na kuitii sauti yake kwa imani kubwa na akamaanisha kwelikweli, akaishia kuwa na maisha ya mahangaiko.

Vijana wetu wanahangaika sana kutafuta maisha bora kupitia mapato watakayopata kila siku lakini, wanaishia kulalamika hali ngumu kutokana na gharama za maisha na hasa kwa wanaoishi sehemu za mijini.

Vilevile, sehemu za vijijini vijana wanahangaika bila kupata suluhisho la kweli. Waliosoma walitarajia kupata kazi za kuvaa tai shingoni lakini wamekwama. Ajira za aina hiyo zimekuwa lulu kiasi kwamba wasomi sasa wamekuwa wengi kupita lugha kutamka na ajira zimekuwa finyu sana.

Baadhi kati ya waliohitimu vyuo vikuu, na vyuo vya-l kati (Technical Certificates' holders) wamepata neema ya kuajiriwa lakini walio wengi wanaishia kutoajiriwa na kubaki wanahangaika kila siku wakitafuta ajira bila kupata.

Hata hivyo, wako baadhi ambao wamepata fursa za kuajiriwa lakini wanakumbwa na changamoto mbalimbali kiasi cha kupoteza ajira zao. Kimsingi, ni kutokana na sababu kadhaa ambazo pengine ni nje ya uwezo wao. Mathalani karibu wengi tumetoka kwenye familia ambazo hazikuwa na uelewa wa kina kuhusu Mungu wa kweli ambaye sisi tumebahatika kumfahamu na kumwabudu.

Yeye aliyehai na kwamba ndiye aliyetuumba kwa kutumia udongo na baadaye kumpulizia binadamu aliyemuumba pumzi ya uhai akapata-kupumua na kuwa nafsihai.

Wahenga wetu wa kale kupitia ukoo au koo tulipozaliwa kwa njia za kibailojia kutoka viuno vya baba kupitia 'matumbo ya mama'; tukawa binadamu na kufungamanishwa na ukoo husika kulingana na mahali tulipozaliwa.

Kwa kuwa mababu na mabibi zetu kupitia kutomfahamu Mungu aliyeziumba mbingu na ardhi; walijiungamanisha na miungu mingine kinyume na Mungu wa kweli. Kujua au kutokujua, yote tisa, kumi ni machukizo makubwa kwa Mungu wetu; ambaye ni Mungu mwenye wivu sana kiasi cha kuamsha ghadhabu yake ambayo ni vigumu kuikwepa.

Maandiko matakatifu yanatuonya kwamba: Mungu hupatiliza wana 'uovu' wa baba zao kizazi cha tatu na cha nne (Kutoka 20:5). Hivyo, tunatahadharishwa kutoisujudia wala kuitumikia miungu mingine kwa sababu Mungu aliyehai hafungamanishi na vitu vingine.

Ukiangalia waliofanya uovu ni baadhi ya mababu zetu lakini 'wana' katika kizazi cha tatu na nne ndio wanaopatilizwa kwa 'uovu' uliofanywa na 'babu/bibi' zetu.

Hili hatuwezi kulikwepa maana ni kanuni aliyoiweka Mungu mwenye haki na hukumu zake ni adili. Sasa kijana aliyesoma lakini anatoka kwenye familia zenye ukoo wenye 'madhababu' waliyoyatumia 'babu/bibi kuiabudu miungu yao na kutoa sadaka mbalimbali kiwemo za kumwaga damu.

Walipokuwa wakifanya hivyo, hawakuwa na ufahamu kuwa walichokuwa wanakifanya ni kinyume na mapenzi ya Mungu. Kwa uelewa wangu mdogo kuhusu elimu ya kiroho (dini); kuabudu miungu' mingine na kuitolea sadaka ni machukizo makubwa kwa Mungu wa kweli.

Waisrael, kwa nyakati tofauti, waliadhibiwa sana mpaka wengi wakipoteza uhai kutokana na machukizo kama hayo ambayo ni machukizo kwa Mungu tunayemwamini.

Nikirejea kwa vijana wetu wanaohangaika kutafuta ajira huku wamemaliza masomo yao vyuo vikuu na vyuo vingine bila kufanikiwa; wakati huo ni wachache sana wanaofanikiwa kuajiriwa lakini baadhi yao pia hawafiki mbali wanaishia kupoteza ajira zao.

Tukifuatilia kwa ukaribu tutagundua pengine ni matokeo ya 'uovu' ulifanyika enzi hizo na kumpelekea Mungu kutuadhibu kupitia kizazi cha tatu na cha nne.

Isitoshe, baadhi yetu yawezekana tulishiriki kwenye ibada za ukoo/koo na kuiabudu miungu mingine; kwa kutokujua athari zake kwa maisha yetu ya baadaye. Ukifuatilia baadhi ya wanaopata ajira lakini wanafukuzwa kazi: henda sababu zikawa ni ulevi uliokithiri, kutowajibika ipasavyo, kutokuwa na nidhamu nzuri au kukosa usikivu na kutii taratibu za kazi hadi kufanya kazi chini ya viwango.

Kadhalika, wapo ambao hawakupata ajira za moja kwa moja lakini wakaona wajiajiri wenyewe (wajasiliamali) wengine kuajiriwa katika sekta binafsi.

Vilevile, iwapo kuna wajasiliamali ambao historia yao inaonyesha wametoka kwenye koo zilizofanya matambiko na kuabudu miungu mingine; watakumbwa na ghadhabu ya Mungu kutokana na uovu waliufanya na babu/bibi hususani muda ukifika kizazi cha tatu na cha nne kitakumbana na changamoto lukuki kwenye shughuli zao za kila siku.

Mathalani, wakifanikiwa kupata mikopo, lakini wanahangaika bila mafanikio, wateja wanakuwa wachache. Isitoshe baadhi yao wanaishia kuwakopesha wateja biadhaa au/na huduma wakitegemea kulipwa kadri walivyokubaliana. Lakini, baadhi hawalipi haraka kulingana na makubaliano.

Mwisho inakuwa hasara tupu hadi kufilisiwa kutokana na kushindwa kulipa mikopo/riba. Vijana wengine hawafanikiwi kutokana nafsi/nyota zao kutekwa/kuchuliwa kimiujiza kupitia 'ulimwengu wa roho wenye asili ya 'giza.

Kadhalika, nyakati hizi zinafahamika za kidijiti ambapo matumizi ya simujanja zimeteka mawazo/fikra za vijana wengi, kiasi cha kutowajali wateja.

Mathalani, unaingia kwenye duka unakuta wahudumu wako bize na simu 'wakichati; unasema lakini wao wako kimya hakuna anayekujali.

Mahali fulani, nilikumbwa na hali kama hiyo hadi nikatamka; "Hivi hapa nazungumza na binadamu au ni sanamu?" Ndipo wakazinduka na kusema samahani baba nikawajibu mbarikiwe nikaondoka.

Hali kama hiyo ni kawaida sehemu nyingi za biashara siku hizi. Ule usemi "mteja ni mfalme" hawana mazoea nao na kuufanyia kazi.

Ni kizazi cha kidijiti hakina mazoea na lugha rafiki kwa wateja bali wameishajiweka kwenye mazingira ya 'kuchati muda mrefu; kwa hali hiyo ni kuwafukuza wateja.

Lakini wapo wenye mafanikio mazuri ukichunguza unakuta ni 'wacha Mungu' hivyo wanayo hekima ya Mungu inayoambatana na ujasiri/kutokata tamaa hadi kuitumia lugha nzuri/rafiki kwa wateja na kujenga 'urafiki-tija' hadi kushikamana nao kwenye shughuli za kila siku: hiyo ndiyo siri kubwa kwa mafanikio yao.

Kadhalika, wapo wanaokwama katika shughuli zao sababu ya tabia zao zinakuwa mbaya mathalani, kutotii maelekezo ya wazazi au/na waangalizi ikiwemo walimu wao.

Inafika wakati mzazi anatoa tamko lisilotarajiwa ambalo linapelekea mtoto kulaaniwa au niseme kutobarikiwa.

Mwisho, vijana wanaishia kutangatanga bila mafanikio kulingana na kile kilichotoka kwenye vinywa vya wazazi wake; baba au mama. Kwa kiasi fulani, wapo wanaofanikiwa katika kufanya biashara zao lakini wanaishia kutumia mapato kianasa na mwisho kutenda 'maovu' ambayo ni machukizo kwa Mungu.

Hivyo hawamchi na kumpa Mungu utukufu kutokana na vifungo vilivyowanasa kutokana na misingi mibovu kwenye koo zao kupitia madhabahu zinazotumika kuiabudu na kuitii miungu mingine iwe ni mizimu au sanamu.

Hata hivyo, vijana wetu katika wingi wao na wenye tabaka mbalimbali ikiwemo makabila mbalimbali na tamaduni na uelewa tofauti, ni vigumu kwao kuweza kuchomoka kwenye mitego ya aina hiyo katika ulimwengu wa kiroho mpaka mhusika apate Neema ya kweli ya Mungu.

Uzoefu unaonesha kuwa vijana wengi wanajikita katika uovu kupitia unywaji pombe uliokithiri, kuvuta sigara hata kulowea kwenye dawa za kulyevya. Bahati mbaya nafsi na vinywa vyao kuna roho za uongo/udanganyifu uliokithiri hivyo kutotii hadi kuwadharau watu wazima hasa wenye umri mkubwa (adabu imepotea).

Mfano, tulipanda mabasi mwendokasi (DRT-buses) na watu wazima wengi tulikuwemo kwenye hicho chombo cha kusafirisha abiria; tukiwa tumesimama (wachache wetu walikuwa wamekaa). Mtu mzima mwenye umri zaidi ya miaka 80 akaingia kwenye basi hilo na kukuta viti vimejaa huki vijana kadhaa wakiwa wamekalia viti.

Mtu mzima aliyekuwa amekaa akawashutua vijana kwa kuwaambia: jamani huyo mzee aliyesimama hamumuoni? Ndipo tukasikia baadhi wanajibu: Mjini (Dar es Salaam) hakuna wazee. Mwisho wa uzee Chalinze!

Kwa mtazamo au welekeo huo, vijana wetu wamepotoka kimaadili na kwenda kinyume na tamaduni zetu ambazo ni nzuri, zinastahili kuendelezwa.

Hata kama kuna wazee wanaoendekeza ujana, wakiamini uzee mwisho Chalinze na kufanya mambo ambayo usingeyatazamia kuona yanafanywana mtu huyo mzima, basi huku pia nikenda kinyume na maadili.

Vijana ni vyema wafahamu kuwa wanapanda mbegu mbaya, lakini wakibahatika kuufikia umri mkubwa yanayowatoka vinywani mwao, yatawakumba hivyo hivyo, kubaki wanalalamika maisha magumu hadi uzeeni.

Ndio maana nasema unapolia maisha magumu, jiulize wewe unachangiaje?

Itaendelea.



# Mengi yamefanyika miaka 60 ya Muungano Tanzania

**Na Hellen Mwango**

MAADHIMISHO ya miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yalifanyika nchini kote wiki iliyopita Aprili 26, huku yakionesha kwamba kumekuwa na mafanikio makubwa kisiasa, huduma za kijamii, ulinzi na usalama, kiuchumi na kimazingira.

Katika kipindi hicho chote kumekuwa na mapito ya changamoto za hapa na pale, lakini manufaa au tuseme faida ni nyingi, hali ambayo inawafanya Watanzania kutembea kifua mbele.

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliasisiwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliyekuwa Rais wa kwanza wa Tanganyika na Rais Sheikh Abeid Amani Karume Rais wa kwanza wa Zanzibar.

Ilikuwa ni kipindi ambacho nchi nyingi za Afrika zilikuwa zimetoka kupata uhuru au ziko katika harakati za kupata uhuru huku Kukiwa na mawazo mengi ya kuunganisha Bara la Afrika.

Muungano ulifanyika Aprili 26, 1964 na kuzaa jina la Tanzania na tunapoadhimisha miaka 60 sasa unaendelea kuwa muungano wa pekee Afrika na dunia nzima kwa ujumla.

Zipo nchi nyingi Afrika, Ulaya na Asia ambazo zilijaribu kuungana lakini safari ya muungano wao iliishia ukutani.

Mafanikio ya muungano huu, kwa maana ya maendeleo ambayo nchi umepata huku sehemu kubwa ikichagizwa na Muungano yapo mengi aghalabu katika kila nyanja; elimu, afya, maji, barabara, umeme, chakula cha kutosha pamoja na ustawi wa jamii kwa ujumla.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo katika taarifa yake kwa umma Machi 26, mwaka huu, jijini Dodoma, alibainisha mafanikio lukiki yaliyopatikana katika kipindi hiki cha miaka 60 ya Muungano.

Anasema kudumu kwa Muungano kunatokana na utashi wa dhati wa kisiasa waliokuwa nao waasisi wa Muungano na viongozi ambao wameendelea kuongoza nchi yetu.

Kwamba tumebahatika kuwa na viongozi wa kitaifa ambao wamekuwa na uchungu na Muungano wakitaka kuona unasimama muda wote.

Ni kutokana na uongozi wetu uliwezesha pia vyama vya siasa vya Tanganyika African National Union (TANU) na Afro Shiraz Party (ASP) kuungana Februari 5, 1977 na baadaye kuunda Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Kuunganishwa kwa vyama hivi kuliongeza ari ya umoja na ushirikiano kati ya watu wa Tanganyika na Zanzibar na muungano wa vyama hivyo ni nguzo muhimu katika kujenga mfumo wa kuwa na vyama vya siasa vya kitaifa, kukuza demokrasia, uhuru wa kutoa maoni na uwazi katika uendeshaji wa shughuli za kisiasa," anasema Jafo.




### ELIMU

Akizungumzia kuhusu elimu, Waziri Jafo anasema, shule za msingi zimeongezeka kutoka shule 3,270 kipindi cha Muungano hadi shule 20,562 mwaka huu.

Anasema kati ya hizo, shule za Serikali ni 18,012 na za binafsi ni 2,550.

Kwa upande wa Shule za Sekondari pia anasema zimeongezeka kutoka shule 41 hadi shule 6,511 mwaka huu, kati ya hizo, 4,892 ni za Serikali na 1,619 ni za binafsi.

### AFYA

Kwa upande wa huduma za afya, Waziri Dk. Jafo anasema zinaendelea kuimarika kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali katika kipindi chote cha Muungano.

Anasema kutokana na uwekezaji huo, vituo vya kutolea huduma za afya ngazi zote vimeongezeka kutoka vituo 1,343 kwa mwaka 1960 hadi vituo 9,662 mwaka huu.

Kati ya vituo hivyo, anasema zahanati ni 8,043, vituo vya afya 1,176 hospitali za halmashauri 171, hospitali zenye hadhi ya wilaya 182, hospitali za rufaa za mikoa 28, hospitali zenye hadhi ya mkoa 34, hospitali tano za rufaa za kanda, hospitali zenye hadhi ya kanda 11, hospitali sita maalum, hospitali ya taifa moja na hospitali maalumu za taifa sita.

"Mfanikio mengine yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 60 ya Muungano ni kuimarika kwa upatikana wa huduma za maji, umeme na mtandao bora wa barabara. Upatikanaji wa maji vijijini umeongezeka kutoka asilimia 32 mwaka 2000 hadi asilimia 77, kwa mwaka 2022," anasema.

### HUDUMA ZA JAMII

Katika kipindi chote cha miaka 60 ya Muungano, Dk. Jafo anasema Serikali zote mbili zinaendelea kuweka mazingira wezeshi na rafiki kwa wananchi wa pande zote mbili kufanya kazi kwa uhuru na amani.

Hali hii inaiwezesha wananchi wote kuendelea kujitosheleza kwa chakula na kwamba inaongezeka kutoka asilimia 90, mwaka 2000 hadi 124 mwaka 2022.

### UHUSIANO

Akizungumzia uhusiano, Waziri Jafo anasema undugu na uhusiano wa wananchi unaendelea kuimarika huku wananchi wa pande zote mbili wakiungana katika misingi ya ndoa na kujenga urafiki katika uendeshaji wa shughuli za kibiashara na kijamii.

Anasema uhusiano huo unawaongezea Watanzania uhuru wa kuishi katika eneo la upande wowote wa Muungano, kupunguza migawanyiko ya kijamii na kuondoa hisia za ukabila na ubaguzi miongoni mwao.

### UCHUMI

Waziri Jafo anaendelea kuelezea eneo la uchumi kwamba, tangu kuasisiwa kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Tanzania ina mafanikio makubwa kiuchumi na hasa kwa kuzingatia kwamba Muungano umepanua soko huku matumizi ya sarafu moja yakiwa chachu ya kukuza biashara na kuimarisha uchumi.

Aidha anasema takwimu zinaonesha kuwa mwenendo wa ukuaji wa uchumi katika kipindi cha miaka 60 ni wa kuridhisha na kwamba Pato Ghafi la Taifa linaendelea kukua kutoka Sh. Trilioni 156.4 kwa mwaka 2021 hadi kufikia Sh. Trilioni 170.3, kwa mwaka 2022.

Pia, anasema Pato la Taifa kati ya mtu na mtu linakua na kuongezeka mwaka hadi mwaka na kufikia wastani wa Sh. 2,844,641 (sawa na Dola za Marekani 1,229.1), mwaka 2022 kutoka wastani wa Sh. 2,708, 999 (sawa na Dola za Marekani 1,173.3 kwa mwaka 2021.

"Hali hii imewezesha nchi yetu kuingia kwenye kundi la nchi zenye Kipato cha Kati cha Chini, " anasema.

### MAZINGIRA

Tangu kuasisiwa kwa Muungano, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais inatekeleza na kuratibu shughuli ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira ili kuhakikisha matumizi sahihi ya rasilimali asili na maendeleo endelevu kwa ajili ya kizazi cha sasa na kizazi kijacho.

Idara ya Mazingira ilianzishwa mwaka 1992 ikiwa ni juhudi za Serikali kuhimiza uhifadhi na usimamizi wa mazingira nchini kama ilivyohimizwa na Azimio la Rio, mwaka 1992 linalozitaka nchi zote duniani kutambua uhusiano uliopo kati ya maendeleo na mazingira.

Jafo anasema kutokana na kuanzishwa kwa Idara ya Mazingira, Tanzania ime0ridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa inayohusu uhifadhi na usimamizi wa mazingira katika kutekeleza Azimio la Rio la mwaka 1992.

Hata hivyo, Tanzania iliandaa Mpango wa Kwanza wa Taifa wa Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (National Environmental Action Plan - NEAP), 1994.

Anasema tangu wakati huo, Sera ya Mazingira ya 1997, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191, programu, mikakati, mipango na miongozo mbalimbali ya kitaifa ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira imeandaliwa na kutekelezwa.

Katika utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, jumla ya Sheria Ndogo 326 zimeandaliwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika mikoa ya Dodoma (15), Kilimanjaro (7), Mbeya (57), Mtwara (69), Morogoro (53), Pwani (59) na Ruvuma (66).

Waziri Jafo anaendelea kueleza mwaka 2012 hadi mwaka huu, vyeti 2,812 vya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na vyeti 1534 vya ukaguzi wa mazingira vilitolewa kwa miradi mbalimbali.

Anasema vyeti 17 vya tathmini ya mazingira kimkakati vilitolewa kwa ajili ya kuandaa na kutekeleza sera, mipango na miradi ya kimkakati.

Hata hivyo, anasema Serikali inaendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 ambapo mafanikio makubwa yamepatikana katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira ikiwa ni pamoja na kuratibu utekelezaji wa Kampeni ya Upandaji Miti nchini ambapo kila Halmashauri ya Wilaya ilielekezwa kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka.



## Kurunzi

Na Dk. Reubeni Lumbagala | 0620 800 462

# Masoko haya ya kisasa Jiji la Tanga ni fursa muhimu



Mchoro wa soko la Mlango wa Chuma

Juhudi za kuinua uchumi na kuboresha hali ya maisha ya wananchi zinahitaji mikakati inayotekelezeka na inayogusa maisha ya watu moja kwa moja. Ni muhimu kwa viongozi na wananchi kushirikiana kwa pamoja ili kutimiza azma hiyo yenye mustakabali mwema kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Zipo sekta nyingi ambazo zinachangia maendeleo ya uchumi, mojawapo ni sekta ya masoko. Masoko yanatoa fursa kwa wafanyabiashara na wajasiriamali kuuza bidhaa na huduma ambazo zinachangia kuinua uchumi na kuboresha hali za uchumi za wananchi.

Mikoa, wilaya, miji na vijiji vingi hapa nchini vina masoko ambayo yana mchango mkubwa katika ukuzaji uchumi. Kwa mfano, Jiji la Tanga limepata fursa ya mradi wenye lengo la kujenga masoko makubwa na ya kisasa matatu yajulikanayo kwa majina ya Mdandini, Mlango wa Chuma na Samaki Kasera.

Lengo la hatua hiyo ni kuinua hali za maisha ya wananchi wa Tanga Mjini, mkoa wa Tanga na Taifa pia.

Kipekee kabisa nimpongeze Mbunge wa Tanga Mjini ambaye pia ni Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu ambaye ni alifanya juhudi kubwa za kuhakikisha masoko ya Tanga Mjini yanajengwa na kuwa bora zaidi ili kupanua wigo wa biashara.

Ummy Mwalimu ni Mbunge wa Jimbo la Tanga Mjini kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM). Aliingia bungeni mwaka 2010 kwa mwamvuli wa viti maalumu hadi mwaka 2020 alipoamua kugombea Jimbo la Tanga Mjini ambapo aliibuka kidedea na kufanikisha kuwawakilishi wananchi katika jimbo hilo kwa kipindi cha miaka mitano, yaani 2020-2025.

Moja ya ahadi ya Mbunge Ummy kwa wananchi wake ilikuwa ni kuhakikisha wafanyabiashara wa Tanga Mjini wanafanya biashara zao katika mazingira mazuri na rafiki ili kukuza uchumi wao na wa Taifa.

Masoko ni moja ya eneo ambalo lina mchango mkubwa katika kukuza uchumi. Kwanza tujiulize soko ni nini na lina faida gani?

Neno 'soko' hurejelea mahali ambapo wanunuzi na wauzaji hukutana kwa ajili ya shughuli za kibiashara au tuseme kubadilishana bidhaa na fedha. Kazi ya soko ni kuwezesha ubadilishanaji wa bidhaa na huduma kufanyika kwa njia ambayo wanunuzi na wauzaji hukutana wao kwa wao.

Uwepo wa soko kunafanya mzalishaji, hususani mkulima kuwa na uhakika wa kupeleka mazao yake. Lakini hapon pia kuna wengi wananufaika; madalali, wachuuzi, lakini pia Halmashauri ya Jiji kwa kukusanya ushuru.

Kutokana na ukweli huo, Mbunge Ummy Mwalimu ameipa nguvu na msukumo mkubwa sekta ya masoko ili wananchi wa Tanga Mjini waweze kunufaika na hatimaye kuboresha hali zao za kiuchumi.

Jimbo la Tanga Mjini lina masoko mengi, mathalani Uzunguni, Kisosora, Majani Mapana, Mlango wa Chuma, Makorora, Mgandini na Ngamiani kutaja kwa uchache ambayo yanachangia sana kuongeza mapato ya ndani ya halmashauri na ya nchi pia kupitia ushuru na kodi zinazolipwa na wafanyabiashara.

Ili kuongeza hamasa kwa wafanyabiashara kulipa ushuru na kodi kwa hiari, mazingira wanayofanyia biashara yanapaswa kuboreshwa na kuwa bora zaidi ili wafanyabiashara waone tija ya kuendelea kulipa kodi serikalini.

Inapotokea wafanyabiashara wanalipa kodi zao, lakini hakuna uboreshaji wa mazingira yao ya kufanyia baishara, wanavunjika moyo wa kuendelea kulipa kodi na hvyo kuilalamikia serikali yao kwa kushindwa kuwahudumia ipasavyo.

Kutokana na umuhimu wa uboreshaji wa mazingira ya wafanyabishara wakiwemo wa masokoni, Mbunge Ummy Mwalimu amefanya juhudi kubwa za kuboresha mazingira ya masoko kwa kuhakikisha masoko ya Tanga Mjini yanaboreshwa na kuwa ya kisasa zaidi ili kuchochea uchumi wa wananchi na Taifa.

Serikali ilibuni mradi wa uendelezaji miji kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya (EU), mradi huo unajulikana kwa jina la Green & Smart Cities. Mradi huu unazinufaisha majiji ya Tanga, Mwanza na Halmshauri ya Ilemela.

Kwa Tanga Jiji, mradi huo utakuwa na manufaa kwa kuwa utajenga masoko ya kisasa ya vyakula kutoka mashambani, soko la uchakataji wa samaki, miundombinu ya kijani, kudhibiti maji taka, kuboresha maji safi na kuhakikisha taka zote zinzozalishwa jijini Tanga zinachakatwa na kutengeneza bidhaa mbalimbali.

Sekta ya masoko katika jimbo la Tanga Mjini itanufaika moja kwa moja kwani kupitia mradi wa Green & Smart Cities kama nilivyotangulia kusema mwanzoni ambapo mradi huu utaboresha masoko matatu ya Mlango wa Chuma, Mgandini na lile la Samaki Kasera.

Katika Bajeti ya 2024/2025, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) imeshaidhinisha utekelezaji wa miradi huu. Kwa mantiki hiyo, kuanza kwa bajeti mpya Julai Mosi, 2024, kunatoa fursa ya ujenzi wa masoko hayo matatu ambayo kwa pamoja yatagharimu shilingi bilioni 52.5 ambayo ni matokeo ya juhudi kubwa zinazofanywa na Mbunge Ummy Mwalimu kwa wananchi wake wa Tanga Mjini kuinua sekta ya masoko.

Kutokana ya masoko haya kujengwa kisasa na kuwa makubwa kuliko ilivyo sasa, kunatoa fursa kwa wafanyabiashara wengi kupata vizimba vya kufanya biashara kuliko idadi ya sasa. Ongezeko la wafanyabiashara katika masoko haya matatu kunaongeza ajira kwa wananchi na hivyo kuboresha uchumi moja kwa moja.

Vilevile, masoko haya yataongeza makusanyo ya ushuru na kodi kutoka kwa wafanyabiashara. Mradi wa masoko haya matatu yanategemewa kuongeza makusanyo na hivyo kuimarisha mapato ya ndani ya Halmashauri ya Jiji la Tanga na nchi kwa ujumla.

Kuinua sekta za kilimo na uvuvi. Masoko haya yatakuwa chachu kwa wakazi wa mkoa wa Tanga kuongeza uzalishaji katika kilimo na uvuvi kwani kutakuwa na masoko ya uhakika kwa ajili ya mazao ya kilimo na uvuvi. Ikumbukwe kilimo na uvuvi ni sekta muhimu kwa uchumi wa mkoa wa Tanga. Ujio wa masoko haya ya kisasa ya Mgandini, Mlango wa Chuma na Samaki Kasera, kuna mchango wa moja kwa moja katika kuinua kilimo na uvuvi.

Pamoja na hayo, pia masoko haya yatakuwa chachu ya uboreshaji wa sekta nyingine kama vile elimu, afya, maji, miundombinu. Mafanikio ya sekta moja yanagusa pia sekta nyingine. Ongezeko la mapato kutokana na masoko haya, yataijengea uwezo wa kimapato Halmashauri ya Jiji la Tanga na hivyo kuwa na kumudu kuboresha sekta hizo kupitia mapato ya ndani na hivyo kuchochea maendeleo zaidi kwa wakazi wa Tanga na Taifa kwa ujumla.

Ni muda mwafaka sasa kwa wakazi na wananchi wa Jiji la Tanga kuchangamkia fursa ya vizimba katika masoko haya matatu pindi yatakapokamilika ili kuongeza ajira na kukuza uchumi wao. Wakulima na wazalishaji wengine wa bidhaa wa ndani na hata nje pia wazidi kufanya shughuli zao wakilenga kunufaika na masoko haya. Halmashauri ya Jiji la Tanga iendelee kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha masoko mengine ili kukuza biashara.

Mbunge Ummy Mwalimu aendelee kutafuta fedha ndani na nje ya nchi ili kuboresha zaidi masoko jijini Tanga ili kuchagiza zaidi maendeleo ya wapiga kura. Kwa hakika, masoko yote Tanga Mjini yakiboreshwa na kuwa ya kisasa, yatasaidia sana kuboresha hali za kiuchumi za wananchi wa Tanga. Juhudi zilizofanywa na Mbunge Ummy Mwalimu za kuinua sekta ya masoko Tanga Mjini ninapaswa kuungwa mkono na wananchi kwa kuchangamkia fursa hiyo muhimu ya kiuchumi kwa maendeleo endelevu.

***Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***



Paul Mng'ong'o

KLINIKI YA FIKRA

# MAMBO KADHAA KUHUSU FEDHA - 4




Wiki kadhaa zilizopita tulilianza somo hili lenye makusudi ya kuimarisha ufahamu wetu kuhusu fedha. Leo tunaendelea na sehemu ya tatu. Ni muhimu kufahamu mambo haya kwa undani kama una malengo ya kukua kifedha.

Mambo haya ninayokuletea hapa ni sahihi kabisa na yamehakikiwa na kutolewa pia na mwongozo wa nyenzo ya kufundishia elimu ya fedha uliotolewa na Wizara ya Fedha. Karibu tuendelee na safu hii sehemu ya nne kwa faida yako na ustawi wa jamii yetu.

### UWEKEZAJI UWEKEZAJI NI NINI?

Uwekezaji ni kununua mali kwa madhumuni ya kupata mapato katika siku zijazo au kuiuza baadae kwa gharama ya juu kwa ajili ya kupata faida. Uwekezaji unaweza kuwa katika hali ya mali kama vile mifugo (ng'ombe, mbuzi, kuku), ardhi, mazao, kulima miti, vyumba vya kukodisha, majengo, vito vya thamani (kama dhahabu,almas, tanzanite), biashara (kama maduka, bodaboda) au dhamana (kwa maana ya hisa na hatifungani) zinazotoa faida.

### AINA ZA UWEKEZAJI

### 1. HISA

Hisa ni sehemu ya umiliki wa kampuni. Mwekezaji anayenunua hisa za kampuni, ananunua haki ya kumiliki kampuni hiyo. Stahili za mwanahisa ni pamoja na kushiriki katika kutoa maamuzi ya kampuni katika mikutano mikuu ya wanahisa; kupata gawio litokanalo na faida ya kampuni; na kuuza hisa zake kwa faida pale ambapo kuna ongezeko la thamani ya hisa.

Bei ya hisa za kampuni zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa hubadilika kwa wakati kulingana na nguvu ya soko, ambapo thamani ya hisa huweza kuongezeka au kupungua. Hivyo ni muhimu mnunuzi wa hisa kujiridhisha na mwenendo wa utendaji wa kampuni kabla ya kuwekeza kwenye hisa zake.

### FAIDA YA KUWEKEZA KWENYE HISA

(i) Kupata gawio kutokana na faida ya kampuni;

(ii) Ni moja ya njia ya kuweka akiba kwa matumizi ya baadaye;

(iii) Kupata fursa ya kutoa maoni kwenye mkutano mkuu wa kampuni; na

(iv) Hisa zinaweza kutumika kama dhamana (collateral) ya kupata mkopo.

Katika uwekezaji wa hisa, ni muhimu kuwekeza kwenye hisa za kampuni zilizoorodheshwa katika soko la hisa kutokana na faida mbalimbali zikiwemo:

(i) Unafuu wa kodi ya zuio kwenye gawio ya asilimia 5 kwa kampuni zilizoorodheshwa kwenye soko la hisa ukilinganisha na asilimia 10 kwa zile zisizoorodheshwa; na

(ii) Hakuna kodi ya ongezeko la thamani ya hisa za kampuni zilizoorodheshwa kwenye soko la hisa ikilinganishwa na asilimia 10 kwa zile zisizoorodheshwa kwenye soko la hisa.

### II. HATIFUNGANI

Hatifungani ni hati ya deni ambalo Serikali au kampuni hukopa kutoka kwa wawekezaji/umma kwa makubaliano maalumu ya kimkataba na huwalipa wawekezaji riba (coupon). Aidha, baada ya kupevuka kwa hatifungani, yaani baada ya muda wa makubaliano ya ukomo wa uwekezaji kufika, wawekezaji hurejeshewa pesa zao (Principal Amount).

### AINA KUU ZA HATIFUNGANI

(a) Hatifungani za Kampuni (Corporate Bonds); na

(b) Hatifungani za Serikali (Government Bonds)

(a) Hatifungani za Kampuni (Corporate Bonds);

Hatifungani hizi hutolewa na kampuni binafsi baada ya kupata idhini kutoka CMSA kwa lengo la kupata fedha au kukuza mitaji kwa ajili ya kugharamia shughuli zao za maendeleo. Hatifungani za kampuni hupevuka ndani ya muda ulioainishwa katika waraka wa matarajio. Hatifungani za Kampuni hutolewa kwa umma kupitia soko la awali (primary market) na baadaye kuorodheshwa katika soko la hisa (secondary market), ambapo wawekezeji hushiriki kupitia watendaji wa masoko ya mitaji wenye leseni za Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA). Kampuni mbalimbali zimekuwa zikitoa hatifungani kwa umma kwa lengo la kupata mitaji. Mfano, benki ya NMB, NBC, Standard Chartered, Exim, kampuni ya TMRC n.k. Hadi kufikia Disemba, 2020 hatifungani 16 za kampuni binafsi zimetolewa kwa umma na kuorodheshwa kwenye Soko la Hisa (DSE). Vilevile, kuna Hatifungani za Manispaa (Municipal bonds). Hatifungani hizi hutolewa na Halmashauri za Serikali za Mitaa, Wilaya, Miji, Manispaa na majiji kwa lengo la kupata fedha za kugharamia miradi ya maendeleo, kama vile ujenzi wa barabara, madaraja, shule, hospitali, maegesho ya magari, masoko, n.k.

(b) Hatifungani za Serikali

Hatifungani hizi hutolewa kwa Umma na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) kwa niaba ya Serikali kupitia Soko la Awali (Primary Market) ili kuiwezesha Serikali kupata fedha za kugharamia miradi ya maendeleo. Baada ya mauzo ya awali, Hatifungani hizi huorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) ambapo hatifungani hizi huuzwa na kununuliwa kwa wawekezaji mbalimbali kulingana na nguvu ya Soko. Aidha, hatifungani za Serikali zimegawanyika katika makundi mawili ambayo ni hatifungani za muda mfupi na muda mrefu.

Hatifungani za muda mfupi (Treasury Bills), hizi ni hatifungani ambazo muda wa kupevuka wa uwekezaji ni chini ya mwaka mmoja (siku 35, 91, 182 na 364). Riba za Hatifungani hizi huwa ni asilimia 3.24, 5.21 na 9.17 kulingana na muda, kama zilivyoainishwa hapo juu.

Hatifungani za muda mrefu (Treasury Bonds), Hizi huchukua muda wa kuanzia miaka 2 na zaidi. Kwa Tanzania, hatifungani za muda mrefu huanzia miaka 2, 5, 7, 10, 15, 20 hadi miaka 25. Hizi mara nyingi huwa na riba (coupon rate) ya 7.82%, 9.18%, 10.08%, 11.44%, 13.5% 15.49% na 15.95% kulingana na muda kama zilivyoainishwa hapo juu.

### WANAOSTAHILI KUSHIRIKI KATIKA UWEKEZAJI WA HATIFUNGANI ZA SERIKALI

Wakaazi/wakazi wote wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wanastahili kushiriki katika mnada wa hatifungani za Serikali. Mwekezaji mwenye kiwango cha kuanzia shilingi 1,000,000 kwa hatifungani za muda mrefu na kiasi cha shilingi 500,000 kwa hatifungani za muda mfupi anaruhusiwa kushiriki katika mnada wa hatifungani hizi. Aidha, wawekezaji watashiriki katika ununuzi wa hatifungani za Serikali kupitia kwa wakala wanaotambulika kisheria.

Kama ungependa kupata ushauri au usimamizi wa karibu katika kuishi mwongozo huu, (Unaweza kuwa Taasisi, Kikundi, Kanisa, Umoja, NGO au Mtu binafsi), karibu sana tutashirikiana nawe kwa neema na msaada wa Mungu. Karibu uwasiliane nasi kwa namba 0676055444 au barua pepe mngongopaul@yahoo.com

***Wework Consult - Your Partner in Growth***

***ITAENDELEA WIKI IJAYO……***

# Muungano na uhusiano wa Kimataifa

**Na Mwandishi Maalumu**

MUUNGANO wa Tanganyika na Zanzibar ndio chanzo cha ushirikiano wa Kidiplomasia na Jamhuri ya Watu wa China wakati huo chini ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Sheikh Abeid Amani Karume kwa kushirikiana na Mwenyekiti Mao Ze Dong na Waziri Mkuu Chou en Lai wa China ambao sasa unatimiza miaka 60.

Alama ya Tanzania kwa Taifa la Watu wa China imesimikwa na Mwalimu Nyerere, Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliposhauri na kupigania Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China (The People Republic of China) kujiunga na Umoja wa Mataifa.

Tanzania ilipambana na Marekani mwaka 1973 kuipigania China kuingia kwenye Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa wakati aliyewahi kuwa Rais wa nchi ya Marekani, George Bush 'Senior' alipokuwa Balozi wa Marekani Umoja wa Mataifa na Dkt. Salim Ahmed Salim akiwa Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa.

Mwana Diplomasia huyo aliwezesha nchi ya China kuchukua kiti chake halali cha Umoja wa Mataifa ambacho kilichokuwa kinakaliwa kinyemela na Taiwan, Taifa ambalo lilikuwa jimbo lililoasi toka China kutoka Chama cha Kikomunisti cha China na kujiita Kuomitang chini ya Kibaraka Kai Shekh kuanzia 1947.

Wakati wa kampeni hizo ujumbe wa Tanzania ukiongozwa na Chifu Patrick Kunambi ulihakikisha China inaingizwa UN na kuigaragaza Marekani ambayo ilianza kununua kura za wajumbe kwa kutoa rushwa waziwazi kwa hela ambazo Bush alisema anatoa papo kwa papo. Njama hizo hazikufua dafu kwa diplomasia ya Tanzania, mwishowe China iliingia UN kwa kishindo.

Tanzania ikiwa na mtaji wa nchi zisizofungamana upande wowote (Non Aligned Countries), zilishinda kwa umoja na uwingi wao kwani kwenye Baraza Kuu kura za turufu 'Veto' hazitumiki. Hii ilikua faraja sana kwa China ambayo ilianza kukata tamaa wakati ule wa vita baridi ambapo pamoja kuwa mwanachama mwanzilishi aliwekewa vikwazo na Marekani kwa sababu ya kuiunga mkono Taiwan.

Nyakati hizo historia inatuambia siasa za ulimwengu zilikuwa makundi mawili ya Magharibi ikiongozwa na Marekani na Mashariki ikiongozwa na Urusi na hivyo kuanzisha uhasama ambao Marekani ililipiza kisasi kwa Tanzania kwa kumpigia kura ya Veto mara mbili Balozi Dkt. Salim alipowania Ukatibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na kukataliwa na taifa hilo.

Wakati wa kuiingiza China UN Marekani kwa kutamba kwake akaanzisha msemo wa kebehi kwa mataifa ya Afrika wa 'banana republics' ambao Bush alimaanisha nchi ndogondogo zenye uchumi dhaifu.

Lakini Marekani ikashindwa vibaya pamoja na kumwaga fedha nyingi kwani siku zote palipo na ukweli uongo hujitenga; na ukweli siku zote hushinda.

Kwa kuzingatia hayo China na Tanzania ni marafiki wa damu hivyo hufaana kwa dhiki na faraja.

Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere akiwa mwanafalsafa aliyebobea katika masuala mbalimbali duniani ikiwemo historia, alitambua mapema kasoro iliyokuwepo ya Taifa la Watu wa China kuwakilishwa katika Umoja wa Mataifa na Taifa dogo la Kisiwa cha Taiwan.

Jamhuri ya Watu wa China ilikuwa na jumla ya watu milioni 800 wakati huo na Kisiwa cha Taiwan ambacho kilikuwa kinawakilisha China katika Umoja wa Mataifa kikiwa na jumla ya watu milioni 18.

Kutokana na Muungano wetu kuwa na watu mahiri na wana Diplomasia wabobezi Mwalimu alimwagiza Balozi wetu wakati huo katika Umoja wa Mataifa, Dkt. Salim (ambaye ni Mzanzibari) ahakikishe China inaingizwa Umoja wa Mataifa na kuwa mwanachama wa umoja huo, historia hii imeandikwa mwanzoni mwa miaka ya 1970.

Dkt. Salim alitoa pendekezo hilo kwenye Umoja wa Mataifa na kuwauliza kwa nini Taiwan ikiwa na idadi ndogo ya watu inaiwakilisha China kwenye Umoja huo badala ya China kuiwakilisha Taiwan yenye idadi ndogo ya watu na eneo dogo la kijiografia.

Umoja wa Mataifa ukachukua hatua stahiki kwa kukaa kikao na kujadili mapendekezo hayo ya Serikali ya Tanzania juu ya Jamhuri ya Watu wa China kuwa miongoni mwa nchi wawakilishi katika Umoja huo na takribani nchi 33 zilipiga kura ili kumpata mwakilishi halali kati ya China na kisiwa cha Taiwan, matokeo yake China ilishinda hapo ndipo ilipoanza kujulikana Kimataifa.

Hivyo, China ni wenzetu na historia inajieleza ambapo katika miaka ya 1960 nchi nyingi za Afrika zilikuwa katika vuguvugu la kutafuta uhuru, Tanzania ikiwa miongoni mwao. Wakati huo China ilikuwa katika vita baridi na Marekani na kiuchumi ilikuwa ni nchi masikini.

Hata hivyo, Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere na Rais wa kwanza wa Zambia Kenneth Kaunda walikwenda nchi za magharibi kuomba kujengewa reli kati ya Tanzania na Zambia kwa sababu reli zilizokuwepo Afrika Kusini, Zimbabwe na Msumbiji zilikuwa zikiendeshwa kwa ubaguzi, nchi za magharibi hazikukubali ombi hilo. Lakini walipokwenda China kuomba msaada huo wa ujenzi waliambiwa reli hiyo itajengwa kwa ushirikiano.

Wachina wakashiriki katika ukombozi wa Kusini mwa Jangwa la Sahara ambapo walijenga Reli ya TAZARA iliyojulikana kama Reli ya Uhuru. Mwenyekiti Mao Ze Dong na Waziri Mkuu Chou en Lai wa China walikuwa marafiki wa Mwalimu Nyerere Baba wa Taifa la Tanzania na urafiki huo umedumishwa hadi leo.

China imeimarika na kuwa mshirika mkubwa wa Afrika kiuchumi. Fedha zinazotoka China kuelekea Afrika zimekuwa zikiongezeka tofauti na zamani.

China imekuwa ikitoa misaada na kuwa mfadhili mkuu wa fedha katika kutekeleza miradi mingi ya miundo mbinu ambayo inashuhudiwa Barani Afrika na Tanzania kwa ujumla katika miaka ya hivi karibuni. Hakuna nchi inayoweza kulingana na kiwango chake cha ushirika.

Kutokana na hali hii, biashara inainuka kwa asilimia 20 kila mwaka, katika kipindi cha mwongo mmoja uliopita. Yapo makampuni zaidi ya 10,000 ya China yanayofanya kazi barani Afrika, hiyo ikiwa ni mara nne zaidi ya makadirio ya awali. Inakadiriwa kuwa asilimia 90 ya kampuni hizo ni zile za binafsi katika sekta tofauti huku theluthi moja zikijikita katika viwanda.

Kampuni hizo zinachangia kwa mitaji ya uwekezaji, maendeleo ya usimamizi na ujasiriamali katika sekta mbalimbali Barani Afrika. Kwa kufanya hivyo, zinasaidia kukuza maendeleo ya uchumi wa nchi za Afrika. Tunaamini kuna nafasi ya kuendelea zaidi.

Mbali na viwanda, robo ya kampuni za China zimejikita katika utoaji huduma kwenye biashara na ujenzi. Tayari asilimia 12 za mapato ya viwanda vya Afrika hutokana na kampuni za China, hiyo ikikadiriwa kuwa ni jumla ya dola bilioni 500 kwa mwaka.

Kwa upande wa miundombinu, China imechukua asilimia 50 ya soko la Afrika husuani kwenye uhandisi, ununuzi na ujenzi. Kampuni za China zinapata faida nzuri na kurejesha fedha zao za mtaji kwa muda wa mwaka mmoja au chini ya muda huo.

Kampuni hizo zinalenga zaidi matakwa ya masoko ya Afrika yanayokuwa kwa kasi kuliko kulenga kwenye bidhaa za kuuza au kusafirisha nje ya Afrika. Uwekezaji wao unaashiria ushirikiano wa kudumu kwa Afrika. Kampuni za China zina matumaini ya mustakabali mzuri wa Afrika.

Uwekezaji na biashara Barani Afrika unaofanywa na China unaleta faida kuu za kiuchumi kama vile kubuni nafasi za ajira na taaluma, kubadilishana ujuzi na teknolojia na pia ni ufadhili na maendeleo ya miundo mbinu.

Imani na alama aliyoiweka Mwalimu Nyerere na Sheikh Karume shujaa wa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar pamoja na Muungano, ndio inayotufanya tutembee kifua mbele na kuthaminiwa kwa kiasi kikubwa na Jamhuri ya Watu wa China ambao wakati sisi Aprili 26 2024 ni kumbukizi ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, wao wanaadhimisha siku ya kumbukumbu ya Ushirikiano wa Kidiplomasia wa Tanzania na China kutimiza miaka 60 pia.



**Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Mwenyekiti Mao Ze Dong**

# Watu 50 wafa baada ya bwawa kuvunja kingo



**NAIROBI, Kenya**

TAKRIBAN watu 50 wamefariki dunia nchini Kenya baada ya bwawa kuvunja kingo zake kufuatia mvua kubwa na mafuriko, Afisa wa Shirika la Msalaba Mwekundu amesema.

Watu katika vijiji karibu na Mai Mahiu, yapata kilomita 60 kutoka Mji Mkuu, Nairobi, walisombwa na maji walipokuwa wamelala.

Juhudi za uokoaji zinaendelea kuwatoa watu kwenye tope, huku kukiwa na hofu kwamba huenda idadi ya waliofariki dunia ikaongezeka.

Zaidi ya watu 100 wameuawa katika mafuriko ambayo yameharibu sehemu za Kenya mwezi uliopita.

Sauti ya kishindo iliwaamsha watu alfajiri ya juzi Jumatatu huku wimbi la maji likitiririka kutoka kwenye bwawa lililopasuka la mto eneo la Mai Mahiu.

Wakazi walizungumza juu ya usiku wa juhudi kubwa za kuwaondoa watu kutoka kwa mafuriko na kuwachimba kutoka kwenye matope.

Shirika la Msalaba Mwekundu la Kenya, limejiunga na shughuli za utafutaji na uokoaji, huku Meneja wake wa kushughulikia dharura, Anthony Muchiri, akiambia BBC kwamba idadi ya waliofariki dunia imeongezeka hadi kufikia 50.

"Hili ndilo janga baya zaidi kuwahi kunipata katika taaluma yangu," alisema, akiongeza kuwa siyo tu kwamba nyumba za watu zilisombwa, lakini pia sehemu muhimu ya maisha yao.

Kati ya miili iliyopatikana kufikia sasa, 17 ni ya watoto, Kamanda wa Polisi, Stephen Kirui, alisema akinukuliwa na Shirika la Habari la Reuters.

BBC.

## Shirika la Ndege Kenya lasitisha safari za DRC

**WASHINGTON, Marekani**

SHIRIKA la Ndege la Kenya Airways (KQ), limesitisha safari za ndege kuelekea Mji Mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Kinshasa kwa sababu ya kuzuiliwa kinyume cha sheria kwa wafanyakazi wawili na ujasusi wa kijeshi.

KQ ilitoa tangazo hilo juzi Jumatatu katika taarifa kwenye X zamani Twitter na kusema hawawezi kuendeleza safari za ndege bila wafanyakazi hao na kwamba kusimamishwa kwa safari hizo, kulianza jana Jumanne.

Aprili 19, mwaka huu, wafanyakazi wawili wa KQ, waliwekwa chini ya ulinzi na Uchunguzi wa Kijeshi (DEMIAP) kwa sababu ya madai ya kukosa nyaraka za forodha za mizigo ya thamani, kwa mujibu na shirika hilo la ndege.

Lakini Afisa Mkuu Mtendaji wa KQ, alisema mzigo huo haukubebwa au kukubaliwa na KQ kutokana na kutokamilika kwa nyaraka.

Wakati wa kukamatwa kwao , simu za wafanyakazi hao wawili zilichukuliwa na kuzuiliwa hadi Aprili 23, mwaka huu wakati maafisa wa Ubalozi na timu ya KQ, waliruhusiwa kuwatembelea.

Kampuni ya ndege iliwahimiza wanajeshi wa DRC kuwaachilia wafanyakazi wa KQ kwa familia zao.

Hata hivyo, Serikali ya DRC, haijatoa tamko lolote kuhusiana na hilo. BBC.

# Togo yapiga kura ya wabunge baada ya mageuzi ya kikatiba

**LOME, Togo**

RAIA wa Togo, wamepiga kura kuwachagua wabunge baada ya mageuzi ya kikatiba yaliyosababisha mgawanyiko ambao wapinzani wanasema yanampa Rais Faure Gnassingbe, mwanya wa kuongeza muda wa kuendelea kushika madaraka.

Shirika la Habari la AFP, limeripoti kuwa vituo vya kura vilifungwa saa 12:00 jioni na kura zikaanza kuhesabiwa.

Taarifa ya Tume ya Uchaguzi nchini humo ilisema huenda matokeo ya awali yangeanza kutolewa juzi jioni.

**Makamu wakuu wa mikoa 179 wachaguliwa**

Zoezi hilo ni la kuwachagua wabunge 113 na pia kwa mara ya kwanza, makamu wakuu wa mikoa 179 katika wilaya tano ambao pamoja na madiwani, watachagua baraza jipya lililoundwa la seneti.

Kwa mujibu wa chama tawala cha Gnassingbe, UNIR, hatua hiyo inaifanya Togo kuwa na uwakilishi zaidi, lakini vyama vya upinzani viliwahamasisha wafuasi kupiga kura dhidi ya kile walichokitaja kuwa mapinduzi ya kitaasisi.

**Kampeni zamalizika kabla ya uchaguzi**

Baada ya kupiga kura juzi, Jean- Pierre Fabre, Kiongozi wa chama kikuu cha upinzani, National Alliance for Change, alisema walikuwa na kampeni nzuri ya uchaguzi na kwamba wanalaani kasoro za uongozi uliopo madarakani huku akiongeza kuwa raia wa Togo watafanya maamuzi bora.

Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (Ecowas), ilisema kuwa itatuma timu ya waangalizi nchini Togo kufuatilia zoezi hilo la uchaguzi.

Wakati wa kupiga kura, Tume ya Uchaguzi humo, ilikataa kuruhusu Baraza la Maaskofu wa nchi hiyo kupeleka waangalizi wa uchaguzi kote nchini.

Soma pia:Togo: Wabunge sasa kumchagua Rais katika katiba mpya

Kwa upande wake, shirika la kutetea haki la Amnesty International limetoa wito kwa serikali ya nchi hiyo kukomesha ukandamizaji unaoongezeka.



Raia wa Togo akipiga kura ya kuwachagua wabunge Picha: AFP

**Upinzani Togo haufurahii haki ya kujieleza**

Mkurugenzi wa shirika hilo kwa Afrika Magharibi na Kati Samira Daoud, amesema nchini Togo,sauti za upinzani hazifurahii haki yao ya kujieleza na mikutano ya amani. Daoud ameongeza kuwa imekuwa vigumu kuchangia kwa njia huru kwenye mjadala kuhusu katiba mpya kutokana na uoga wa hatua za kisasi.

Wabunge waliidhinisha nafasi inayofanana na ya Waziri Mkuu

Kura hiyo imefanyika baada ya wabunge mwezi huu, kupiga kura kuidhinisha kuwepo kwa nafasi inayofanana na ya Waziri Mkuu ambayo kwa mujibu wa wapinzani, iliundwa ili kumsaidia Rais Gnassingbe kuepukana na ukomo wa kukaa madarakani.


Tayari Gnassingble (57), ameshashinda katika chaguzi nne ambazo zote zilipingwa na vyama vya upinzani kutokana na kile walichokiita kuwa ni dosari.

Kwa mujibu wa katiba ya awali, Gnassingbe angeweza kugombea urais mwaka 2025 pekee katika muhula mmoja uliosalia.

DW.

# Kiswahili kilivyomheshimisha Shaaban Robert

## ● Uingereza walimpatia hadi uraia wa heshima



Marehemu Shaaban Robert

**Na Mwandishi Maalumu**

MWANAFALSAFA bingwa wa Kiswahili Tanzania na dunia nzima, hayati Shaaban Robert Januari 20 mwaka huu alitimiza miaka 62 tangu aage dunia.

Bingwa huyu wa mashairi, ngano, lugha, usanifu, weledi wa ngeli na mwandishi wa riwaya zilizoteka hisia za wengi duniani, kiukweli si mtu wa kudharau hata kidogo kutokana na ukweli kwamba maandishi yake yote yalikuwa yakilenga kitu muhimu na bado yanaishi hadi leo.

Baadhi ya watu na hasa watunzi wa zamani wa vitabu kama kina Shaffi Adam Shaffi kwa kumtaja mmoja wao, wanajua hata kisa cha mzee huyo kutunga vitabu vyake viwili vilivyoitwa "Kusadikika" na "Kufikirika".

Kwa kudokeza tu, alikuwa amejikita zaidi katika maadili ya Tanzania, Watanzania wenyewe na hasa wale waliokuwa wakisadikika kuwa ni wakombozi wa Taifa hili.

Hakika inaeleweka wazi kuwa katika enzi yake palikuwa na malenga wawili wengine waliokuwa wakichuana naye vikali kwenye mashairi, ngano, lugha, usanifu, weledi, ngeli na umahiri.

Lakini kama alivyosema mwenyewe 'Mtu yeyote aliyetenda tendo bora alikuwa bora', ndivyo ilivyokuwa kwake. Kwani ni Sheikh Shaaban bin Robert pekee ndiye aliyeendelea kuishi mpaka leo hii katika nyanja hiyo pamoja na Tanzania kumuwekea 'mtimanyongo' dhidi ya kumbukumbu kubwa kwa ajili yake zaidi ya ile ya shule ya Sekondari ya Shaaban Robert pekee.

Mshindani wake, Shekh Amri Kaluta Abeid wa Kigoma ana kumbukumbu kubwa iliyowekwa huko Arusha ambapo hadi leo anatamkwa kila wanamichezo wanapojifua kwenye Uwanja uliopewa jina lake jijini humo.

Kana kwamba hiyo haitoshi, jina la Sheikh Amri Kaluta Abeid limeendelea kudumu kwenye mitaa kadhaa nchini Tanzania. Iko mitaa kadhaa nchini inaitwa 'Kaluta'. Hiyo ni kwa kumuenzi mshairi huyo ambaye mwishoni mwa maisha yake alitaka kujiingiza kwenye siasa na dini.

Hatua hii ilimponza na kujiondolea sifa yake kwani alianza malumbano ambayo yalihatarisha umoja wa nchi yetu.

Mshindani mwingine wa Sheikh Shaaban bin Robert alikuwa Padri Mathias Mnyampala ambaye pia iko mitaa kadhaa nchini imepewa jina lake kwa heshima yake.

Huyu naye alikuwa malenga wa haja akipepetana na Sheikh Shaaban bin Robert ingawa kwa kweli hakufua dafu hata kidogo mbele yake.

Naye pia alipojiingiza kwenye masuala ya dini kule Kipalapala, sanaa yake ikapotea miongoni mwa watu kiasi kwamba hata athari yake haikuhisiwa au kuonekana tena kwenye jamii yetu hii mpaka leo.

Kwa mtaji huu basi ni kwamba, Sheikh Shaaban bin Robert amechomoa 'ree' kutoka kwenye jozi ya karata. Ndiyo maana leo hii anajulikana zaidi kwa tungo na usawiri wake wa mambo kiasi ambacho jina lake limevuka mipaka ya nchi yetu hadi huko duniani.

Nathubutu kusema hapa kwamba malenga huyu zaidi ya kutochusha kila anapotajwa, lakini ndiye aliyeifundisha dunia lugha fasaha ya Kiswahili.

Kwa jinsi hii basi uko umuhimu mkubwa wa kumtazama malenga huyu kwa jicho la tatu. Kwani kama leo Tanzania inajivuna kuwa lugha ya Kiswahili inatumika kwenye mikusanyiko ya kimataifa, basi wa kumpa shavu la upendo na la ujasiri mkubwa si mwingine bali ni Sheikh Shaaban bin Robert.

Maandiko yake yasiyochuja wala kuchosha mpaka leo hii, utadhani misahafu au Biblia, ndiyo yaliyoifikisha lugha ya Kiswahili hapo ilipo.

Nitoe sifa zangu kubwa hapa kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan naye kwa kujiunga na watangulizi wake kwa kuamua kuienzi lugha ya Kiswahili kwenye kazi zake za kitaifa na kimataifa na hii imetupa faraja kubwa sisi tunaoiona lugha hii kuwa ni ya thamani na ya upendo mkubwa kwa Tanzania na dunia nzima.

Mwaka 2022 Rais Dk. Samia aliupongeza Ubalozi wa Kudumu wa Tanzania nchini Marekani na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni UNESCO kwa kaundaa maadhimisho makubwa ya kwanza ya Siku ya Kimataifa ya Kiswahili duniani na kusema kuwa wameitendea haki lugha hiyo amabayo ni alama ya uhuru, amani na Umoja.

Akiwahutumia wahudhuriaji wa maadhimisho hayo yaliyofanyika katika Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa jijini New York Marekani Dk. Samia alisema; "Mmefanya kazi kubwa na nzuri ya kupiga nguvu Kiswahili, asanteni sana".

**LUGHA YA UHURU**

Akifafanua kwa nini ameiita lugha ya Kiswahili kuwa ni ya Uhuru, Rais Samia alisema; "Msishangae kwa nini nimeihusisha siku hii na Uhuru, Amani na Umoja, nimefanya hivyo kwasababu Kiswahili kilitumika kama lugha ya ukombozi hasa kusini mwa Afrika na hivyo ilichangia sana kuleta uhuru na umoja."

> **Kuna baadhi ya watu hudhani alikuwa akifasiri kama usemavyo msemo huo. Lakini kiukweli ni kwamba mwenyewe alikuwa akiisifia lugha ya Kiswahili kwa kusema kuwa ijapokuwa ilikuwa bado changa mno wakati huo na isiyothaminika kabisa.**

Pia alieleza namna lugha hiyo ilivyotumika kujenga umoja wa kitaifa na mshikamano na kutatua migogoro katika ukanda wa Afrika Mashariki, Kati na Kusini.

Akizungumzia Kiswahili na Malengo ya Maendeleo endelevu ya Umoja wa Mataifa SDGs Rais Dk. Samia alisema lugha hii ni nyenzo muhimu kwenye utekelezaji wa malengo hayo ya SDGs ifikapo mwaka 2030 na agenda ya Umoja wa Afrika ya mwaka 2063.

"Jamhuri ya muungano wa Tanzania iliunga mkono Azimio la Umoja wa Mataifa lenye namba A/76/L57 la mwezi Mei mwaka 2022 kuhusu lugha nyingi, yaani 'Multilingualism' ambalo lilisisitiza umuhimu wa Umoja wa Mataifa kuzipa kipaumbele lugha ambazo sio rasmi katika Umoja huo kama vile Kiswahili hii ni kwa kuhakikisha lugha hii inawafikia watu wengi zaidi duniani," alipasha Rais Dk. Samia.

Alisema maadhimisho hayo yataendelea kuadhimishwa kila mwaka kama ishara ya kutambua umuhimu wa lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya mawasiliano ya Kimataifa inayokuza ushirikiano wenye mchango katika nyanja mbalimbali za amani, umoja na maendeleo ya mwanadamu.

Pia aliwasihi Watanzania kuitumia lugha ya Kiswahili na siku hiyo kutangaza utamaduni wao. Naam, huyo ndiye Rais wetu anayekipigania Kiswahili hadi huko Umoja wa Mataifa.

Uko utafiti uliofanywa duniani ukionesha kuwa lugha hii ni tajiri yenye maneno matamu na ya kuvutia nyuma ya lugha ya Kiarabu yenye kuongoza kwa utamu huo hapa duniani.

Nakumbuka hapa jinsi Sheikh Shaaban bin Robert alivyoendelea kuipa hadhi lugha ya Kiswahili pale aliposema, "Titi la mama li tamu lau kama la mbwa".

Kuna baadhi ya watu hudhani alikuwa akifasiri kama usemavyo msemo huo. Lakini kiukweli ni kwamba mwenyewe alikuwa akiisifia lugha ya Kiswahili kwa kusema kuwa ijapokuwa ilikuwa bado changa mno wakati huo na isiyothaminika kabisa duniani hapo awali, bado ni lugha tamu mpaka hivi leo.

Kana kwamba Sheikh Shaaban bin Robert alikuwa mtabiri, leo hii, Chuo Kikuu na kikongwe duniani cha Oxford cha nchini Uingereza, kimeanzisha kitivo rasmi cha lugha ya Kiswahili.

Haya ni matunda makubwa ya Sheikh Shaaban bin Robert. Kwani pamoja na kwamba hakuwahi kuishi na kuona akipewa tuzo na heshima kubwa na dola ya Kiingereza, lakini leo hii bado dola hiyo kubwa na kongwe duniani imeendelea kumthamini kwa kuruhusu Chuo chake Kikuu hicho cha Oxford kuanzisha kitivo cha lugha ya Kiswahili.

Kwa taarifa tu ni kwamba Chuo Kikuu hicho cha Oxford cha nchini Uingereza hivi sasa kina umri wa miaka 408 na ushei kikiwa ni moja ya vyuo vikuu vichache vyenye umri huo hapa duniani.

Chuo Kikuu kingine kikongwe ni cha El-Azhar cha Misri ambacho kinaelezwa kuwa kina karne karibu 11 kwa maana ya miaka 1008 tangu kianzishwe.

Nadhani baadhi ya watu kama si wengi hawalielewi hili. Kwamba Sheikh Shaaban bin Robert ni mjumbe wa heshima wa dola ya Kiingereza (Member of British Empire-MBE) tangu alipoanza kuandika vitabu vyake vya lugha tamu, fasaha, tajiri na yenye ulimbwende mkubwa; yaani lugha ya Kiswahili.

Leo hii dola hiyo kubwa au Taifa hilo kubwa na kongwe duniani bado linaendelea kumthamini malenga huyo kwa kuanzisha kitivo cha lugha ya Kiswahili kwenye Chuo Kikuu chake cha Oxford.

Wakati dola hiyo ikimpa heshima kubwa malenga wetu huyo, sisi Tanzania tumelala usingizi wa pono. Tumelala fofo bin fofofo.

Inatia aibu kubwa hata kuona Wabunge wakibishana kuhusu kutumia lugha ya Kiswahili bungeni wakati ni lugha ya kimataifa.

Ama kweli 'Mtume hakubaliki kwao'. Katika hili; vyote viwili hapa ni 'mtume'. Sheikh Shaaban bin Robert ni 'mtume' wa lugha ya Kiswahili. Lakini anachukuliwa wa 'kawaida' kabisa na Taifa la Tanzania ambako ni kwao.

Kadhalika, Kiswahili chenyewe pia ni 'mtume'. Lakini hakikubaliki kwao Tanzania na hasa wanaojifanya kuwa ni wasomi kumbe ni ushamba tu umetawala nafsi zao.

Kibaya zaidi kuna wabunge wanaoliongelea hilo ndani ya Bunge ambalo lina kumbukumbu (Hansard) zisizokufa wala kufutika milele na milele.

Kwa mantiki hiyo basi, ubishani wowote unaohoji uhalali na upendo wa 'mama yetu' lugha ya Kiswahili utadumu milele na milele hadi vitukuu vyetu kama si vilembwe vyetu na vinying'inya vyetu vitaikuta na kuipenda.

Vitabu alivyotunga hayati Shabaan Robert ni pamoja na Almasi za Afrika (1971), Koja la lugha(1969), Insha na mashairi, (1967), Kielezo cha Fasili, (1962), Pambo la Lugha, (1968), Ashiki Kitabu Hiki, (1968), Mashairi ya Shaban Robert, (1971), Sanaa ya Ushairi, (1972), Mwafrika Aimba, (1969), Masomo Yenye Adili, (1959), Mapenzi Bora, (1969) na Tenzi za Marudi Mema na Omar Khayyam(1973).

Vingine ni Utenzi wa Vita vya Uhuru(1961), Almasi za Afrika na Tafsiri ya Kingereza (1960), Maisha yangu na baada ya miaka hamsini, (1949), Adili na Nduguze,(1977) Kusadikika (1951), Kufikirika (1968) Wasifu wa Siti bint Saad (1967), Utu bora Mkulima,(1968), Siku ya watenzi wote (1968), Barua za Shabani Robert 1931-1958 (2002) kiliandaliwa na TUKI kupitia kazi zake, Kielezo cha Insha (1954), Methali na mifano ya Kiswahili, (2007) TUKI ilikusanya kazi zake na kutoa kitabu hiki.

**Kwa ushauri na maoni; 0768 888 787 au 0784 122 020.**

# Wanahip-hop wanaongoza kusaidia jamii duniani

**Na Valensi Mbaga**

BAADHI ya wasanii wakubwa katika hip-hop wameamua kutumia mafanikio yao kuwainua wengine. Wapo wengi lakini si rahisi kuwataja wote hapa. Tunakuletea wachache wanaongoza kusaidia jamii miongoni mwao kutokana na utajiri wao.

Wasanii wa muziki wa hip-hop ambao wametoa muda na kutumia talanta na pesa zao kwa kusaidia jamii ni pamoja na hawa wafuatao.

**1: Drake**

Drake amekuwa msanii anayejikita zaidi kusaidia jamii kuondokana na shida mbalimbali kutokana na utajiri alionao ambao ameupata kutokana na kazi yake ya mziki.

Ukarimu wake ulishika vichwa vya habari mara nyingi haswa, alivutia kila mtu wakati albamu yake ya "Gods Plan" ilipotoka na akaendelea na matumizi ya pesa huko Miami ya michango na kazi ya kusaidia watu. Lakini pia amekuwa akitoa misaada kwa wahanga wa matatizo kama vimbunga, vifaa vya shule na misaada mingine wakati huu wote.


Sean Combs

Mwaka jana tu, Drake alitoa dola milioni 1 kwa shule ya LeBron James' I Promise huko Ohio.

**2: Sean Combs**

Wakati Sean "Diddy" Combs anaweka mawazo yake kwa jambo fulani, ana uhakika wa kulifikia kutokana na jitihada zake za uhisani pamoja na muziki wake.

Kwa mfano, alichangisha dola milioni 2 kwa ajili ya watoto wenye VVU/UKIMWI kwa kukimbia New York City Marathon mwaka 2003.

Pia alitumia laini yake ya mavazi, Sean John kwa Huduma ya Saratani ya Matiti, kuhamasisha na kutafiti na baadaye kutoa fedha za kutibu wagonjwa wa saratani ya matiti.

Anaendelea kutumia mafanikio yake kurudisha fadhila kwa jamii zinazohitaji msaada. Mwaka jana tu, alitoa dola milioni 1 kwa Chuo Kikuu cha Howard, akisema kwamba "asingefika alipo bila msaada wa Washington HBCU".

**3: 50 Cent**

Curtis "50 Cent" Jackson aliwahi kuwaambia Forbes kwamba alijua anataka kujihusisha na kazi ya kusaidia jamii punde tu baada ya albamu yake ya kwanza kuifanya kuwa kubwa.

Mara moja alianza kufanya kazi na mashirika kama Feeding America kusaidia watoto wenye njaa.

50 Cent alipokea tuzo ya mwanamziki bora anayejihusisha na masuala ya kijamii kwa kazi yake ya hisani huko Texas, akiweka kiwango cha juu kwa wasanii wengine wa ulimwengu wa hip-hop linapokuja suala la ufadhili wa jamii.

Akiwa na taasisi yake, G-Unity, 50 Cent anaendelea kusaidia watoto katika maeneo ya mbalimbali kupata mafanikio. Msingi hufanya kila kitu kutoka kwa vifaa vya kuchezea hadi kozi nzima ya shule inayolenga ujasiriamali.


Drake


50 Cent


Akon


Snoop Dogg

**4: Akon**

Orodha yetu ya nyota wa muziki wa hip-hop duniani haijumuishi wale wanaorudisha fadhila ndani ya nchi aliyomo tu, Akon ni mfano mzuri wa nyota anayetumia ushawishi wake kwa manufaa ya kimataifa. Hasa, ameelekeza mawazo yake katika kuleta umeme barani Afrika.

Kwa mpango wake wa Lighting Global, anajaribu kuleta sio umeme tu bali nishati endelevu duniani. Tayari, mamilioni ya Waafrika sasa wana umeme kutokana na mpango huo, na Lighting Global imesaidia kutoa mafunzo kwa ajili ya kazi endelevu.

**5: Snoop Dogg**

Snoop Dogg pia ameipeleka kazi yake ya hisani katika kiwango cha kimataifa na Mind Gardens Project, ambayo husaidia watoto katika miji ya ndani ya Jamaika.

Katika ngazi ya kitaifa, amekuwa mkarimu katika kusaidia programu za michezo kwa watoto ambao hawajapata nafasi kubwa na ameanzisha Ligi yake ya Soka ya Vijana ya Snoop.

Kila mtu kwenye orodha hii (pamoja na mastaa kadhaa wa hip-hop ambao hawakutajwa hapa) wameonyesha maana ya kuipa jamii kipaumbele zaidi na kuthamini utu sio utajiri tu walionao. Itapendeza kuona kwamba wao na wengine kama wao wataendelea kutuonyesha maana ya mafanikio waliyonayo kwa jamii.

# Makocha wa kigeni wanavyovuna fedha bwerere TZ

## Simba na Yanga zinaongoza kufukuza na kukimbiwa



Abdelhak Benchikha

**Na Hamid Yassin**

KWA mara nyingine tena Simba imeachana na kocha wake, Abdelhak Benchikha kwa kile kilichoelezwa kwamba wamevunja mkataba wao kwa makubaliano ya pande zote mbili.

Simba imesema Benchikha ameomba mwenyewe kuvunja mkataba huo kwa madai kuwa anauguliwa na mke wake, hivyo anataka awe karibu naye ili 'amuuguze' vizuri.

Cha kushangazza Benchikha ameondoka na wasaidizi wake wote wawili, Kamal Boujnane na Farid Zemit! Je, hawa nao wanakwenda kumsaidia kuuguza mke wake?

Huyu si kocha wa kwanza kuondoka Simba kwa kisingizio cha kwenda kuwa karibu na familia, wa kwanza alikuwa Sven Vandenbroeck aliyetimuka kwenye klabu hiyo Januari mwaka 2021 na kutoa sababu kama hizo lakini kwa mshangao wa wengi ndani ya wiki moja baadaye akaibukia Morocco kwenye timu ya FAR Rabat.

Ndani ya miaka hii sita Simba imefundishwa na makocha tisa, huku nane kati yao wakiwa ni wakigeni! Hii si sawa kwa mustakabali wa klabu yoyote yenye malengo chanya ya kufanikiwa kwenye medani ya mchezo huu pendwa kuanzia hapa nchini, Afrika na Duniani kwa ujumla.

Januari mwaka 2018 Simba ilimwajiri kocha Mfaransa Piere Lenchantre ambaye aliikuta timu hiyo ina ukame wa mataji ya ndani kwa miaka mitano mfululizo, akafanikiwa kurudidha heshima ya klabu hii kwa kuipatia taji la Ligi Kuu, lakini hiyo haikumsaidia kubaki Msimbazi kwani ilipofika Juni 2018 akatimuliwa!

Julai 2018 Simba ikaingia mkataba na kocha Mbelgiji, Patrick Aussems, huyu akawapatia mataji yote ya ndani, kuanzia Ngao ya Jamii, Kombe La FA na lile la Ligi Kuu sambamba na kuifikisha timu hiyo hatua ya makundi hadi robo fainali.

Lakini ilipofika Novemba mwaka 2019, Aussems alifungashiwa vilago vyake na kuondoka huku akitoa maneno ya kuwaponda viongozi wa klabu hiyo kwamba ni waongo na hawana weledi wa mpira.

Ndipo kocha mwingine Mbelgiji, Sven Vandebboeck akachukua nafasi yake Desemba 2019 ambaye alikaa mwaka mmoja na kuiongoza Simba kutamba tena michuano ya ndani na kuifikisha hadi hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, alipofika Januari 2021 akatimka kwenye klabu hiyo ngonjera kama hizi za Benchikha kwamba anataka kuwa karibu na familia yake.

Simba ikawaleta makocha wengine kwa mtindo wa bandika bandua ambao ni pamoja na Didier Gomezi (Januari 2021 – Oktoba 2021), akaja Pablo Franco aliyedumu toka Novemba 2021 hadi May 2022, akaletwa, Zoran Mac aliyekaa na timu miezi mitatu tu toka Juni 2022 hadi Sptemba 2022 na kukimbia.

Mzalendo Juma Mgunda akakabidhiwa timu ya Simba Septemba 2022 lakini ilipofika Januari 2023 akaondolewa na kupewa majukumu mengine ndani ya klabu hiyo pamoja na kufanya vizuri sana alipokuwa na timu hiyo.

Mikoba ya Mgunda akapewa Mbrazili, Roberto Olivieira Januari 2023 akadumu hadi Novemba mwaka huo 2023 akatimuliwa na kuletwa Mwalgeria Abdelhak Benchikha ambaye amedumu kwa miezi mitano tu na kutimka. Sasa amekumbukwa tena Mgunda kuifundisha Simba hadi mwisho mwa msimu.

Kimahesabu hapa Simba ndiyo iliyoingia hasara kubwa kwani makocha wengi kati ya hao walitimuliwa hivyo iliwapasa kuwalipa gharama za kuvunja mikataba yao.

Ukienda kwa watani zao Yanga, hali ni hiyo hiyo hakuna wa kumcheka mwenzake, nao wamekuwa wakibadili makocha wakigeni kama mashati, hususani wakati wa ufadhili wa uongozi wa Yusuph Manji.



Kostadin Papic



Dusan Kondic

Kabla ya ujio wa Kocha Hans Van Der Pluijm raia wa Uholanzi, tayari aliyekuwa Mwenyekiti wa Klabu ya Yanga Manji, alikuwa ametumia zaidi ya shilingi 690.1 milioni kwa ajili ya kuwalipa makocha saba wa kigeni ambao waliifundisha Yanga kwa vipindi tofauti.

Huku makocha hao saba wa kigeni wakiwa wamepitia mikononi mwa Manji tangu mwaka 2007.

Baadhi ya makocha wa kigeni ambao waliifundisha Yanga ni Mserbia Dusan Kondic ambaye alikinoa kikosi cha timu hiyo katika misimu miwili ya mwaka 2007 / 2008 na 2008/ 2009 huku akiwa na msaidizi wake Spaso Solokouski, kwa pamoja walifanikiwa kuipa Yanga ubingwa wa Ligi Kuu bara mara mbili mfululizo kabla ya kutimuliwa na klabu hiyo mwanzoni mwa msimu wa mwaka 2009/2010.

Ndani ya miezi 18 ambayo kocha Dusan Kondic alitumia kuifundisha Yanga, alivuna jumla ya Tsh 70.1 milioni, huku msaidizi wake Spaco Solo Kovski akilipwa jumla ya Tsh 14 milioni.

Lakini kocha Dustan Kondic aliondoka Yanga, huku akiwa anadai fidia ya Tsh 15 milioni kama madai ya kuvunjiwa mkataba wake na timu ya Yanga.

Pia Spaso Solokovski ambaye alikuwa Kocha msaidizi naye aliidai Yanga fidia ya dola 6,000 sawa na Tsh 9 milioni kama mshahara wake wa miezi 6 iliyobaki.

Katika msimu wa mwaka 2010 /2011 timu ya Yanga ilinolewa na Kostadin Papic ambaye alirithi mikoba ya Mserbia mwenzake Dusan Kondic, lakini hata hivyo Papic alitimuliwa ndani ya miezi minane ya kwanza aliyoifundisha timu ya Yanga, huku akivuna Tsh 60 milioni kwa miezi nane ambayo alikuwa ndani ya klabu hiyo aliyokuwa akipokea mshahara wa Tsh 7.5 milioni kwa mwezi.

Kocha Mganda Sam Timbe alichukua mikoba ya kuinoa klabu ya Yanga Januari 2011, akiwa amerithi mikoba kutoka kwa Mserbia Papic. Lakini kama 'kawa' ilipofika Septemba 2011, Timbe alifukuzwa kazi ya kuendelea kukinoa kikosi cha Yanga baada ya kutoka sare na timu ya Mtibwa Sugar, katika uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro.

Timbe alikuwa tayari ameshaipa Yanga ubingwa wa Ligi Kuu bara katika msimu wa mwaka 2010 / 2011 na kombe la Kagame, huku akivuna kiasi cha Tsh. 90 milioni sawa na dola za Kimarekani 53,000 wakati mshahara wake haukuweza kuwekwa wazi.

Lakini baada ya timu ya Yanga kumfukuza Timbe nafasi yake ikajazwa na Papic kwa mara nyingine tena, lakini hata hivyo Mserbia huyo hakuweza kudumu ndani ya timu hiyo na kufukuzwa kazi ndani ya miezi minne huku akiambulia kiasi cha Tsh 7.5 milioni kama mshahara wa mwezi mmoja pia akidai malimbikizo ya mshahara wa miezi mitatu kiasi cha dola za Kimarekani 15,000 ambazo ni sawa na Tsh 22.5 milioni.

Yanga waliweza kumlipa Mserbia huyo malimbikizo hayo kabla Shirikisho la Soka Duniani (FIFA) kutoa adhabu kwa klabu hiyo.

Hatimaye katika msimu wa mwaka 2012 /2013, Yanga ilimpa timu kocha Mbelgiji Tom Saintfiet baada ya kumfukuza kazi Papic, lakini kocha huyo Saintfiet alidumu ndani ya kikosi cha Yanga kwa siku 80, na kufukuzwa kazi baada ya kuanza vibaya msimu kwa kuambulia kipigo cha mabao 3-0 kutoka kwa Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro.

Kipigo hicho kilisitisha ajira ya kocha huyo huku akivuna kiasi cha Tsh 36 milioni kama mshahara wake wa miezi mitatu wa kuifundisha klabu hiyo, lakini baada ya kuvunjiwa mkataba wake Saintfiet alidai fidia ya Tsh 18 milioni sawa na dola za Kimarekani 12,500.

Kocha Mdachi Ernest Brandts alikabidhiwa mikoba ya kuiona timu ya Yanga baada ya kumfukuza kazi Saintfiets. Lakini Brandts alidumu kwa msimu moja wa mwaka 2013 /2014, sababu kubwa ya kufukuzwa kwa kocha huyo ni kutokana na timu ya Yanga kukosa ufanisi, pamoja na kutoridhishwa kwa uchezaji wa timu nzima, pia kufungwa mabao 3-1 na Simba katika mechi ya 'nani mtani Jembe'.

Brandts alikuwa akilipwa mshahara wa Tsh 17.6 milioni kwa mwezi huku akivuna kiasi cha Tsh 211.2 milioni ndani ya miezi 12 aliyo kaa Jangwani.

Kocha Hans Pluigm alikabidhiwa mikoba ya Ernest Brandts lakini hata hivyo Pluigm alidumu katika timu ya Yanga kwa kipindi cha miezi 6 katika msimu wa mwaka 2013/2014 na kuvuna kiasi cha Tsh. 108 milioni huku akipokea mshahara wa Tsh. 18 milioni kwa miezi 9.

Katika msimu wa mwaka 2014/15 Yanga ilinolewa na kocha Mbrazil Marcio Maximo ambaye aliwahi kuwa Kocha wa timu ya Taifa yaTanzania 'Taifa Stars' kuanzia Juni 2006 hadi Juni 2010, hata hivyo, naye alifukuzwa katika klabu ya Yanga, ingawa alikuwa akilipwa kiasi cha Tsh. 19 milioni kwa mwezi sawa na dola za Kimarekani 12,000. Mikoba yake ikachuliwa tena na kocha Hans Van Der Pluijm ambaye hata hivyo hakudumu sana akatimkia Uarabuni akiongozana kocha mzalendo Charles Boniface Mkwasa aliyekuwa anamsaidia pale Yanga.

Baada ya hapo wakafuata kina Mzambia George Lwandamina (2016- 2018), Mkongomani Mwinyi Zahera ( 2018 – 2020), Mbelgiji Luc Eymel (2020), Msebiea Zlatko Krmpotic (2020), Nasreddin Nabi na sasa Miguel Angel Gamond.

# Leicester kuonyesha tena maajabu EPL?

**Na Valensi Mbaga**

LEICESTER City (The Foxes) ambao walishinda Ligi Kuu ya nchini England ( EPL )msimu wa 2015/16 na baadaye kushuka daraja mwishoni mwa msimu wa 2022/23, sasa wamerudi tena katika Ligi hiyo ya EPL baada ya kushinda kwa kishindo cha bao 3-0 dhidi ya Preston.


The Foxes bado wanaweza kufikisha alama 100 ikiwa wataishinda Blackburn nyumbani siku ya mwisho ya msimu, na kuangazia kampeni yao bora kwa jumla wanaporejea ligi kuu baada ya kukosekana kwa mwaka mmoja tu.


Wakati kikosi kikiwa kimebadilika kwa kiasi fulani mwaka huu kufuatia kushuka daraja na kuteuliwa kwa Enzo Maresca kama kocha mkuu, baadhi ya majina yanayofahamika yanabaki kwenye kikosi cha Leicester hasa mfungaji bora Jamie Vardy, ambaye amefunga mabao 18 msimu huu licha ya kuingia akitokea benchi lakini mara nyingi alianza.

Kiernan Dewsbury-Hall amefikisha mabao kumi na mbili, huku makinda kama Wout Faes, Jannik Vestergaard na Ricardo Pereira wamekuwa wachezaji wa kutazamwa zaidi kutokana na kiwango chao.

Maresca, ambaye aliteuliwa kwa mkataba wa miaka mitatu msimu uliopita wa kiangazi, alikuwa sehemu ya wakufunzi wa timu ya vijana ya Manchester City kuanzia 2020 kwa mwaka mmoja, kabla ya kuchukua wadhifa wake wa kwanza katika klabu ya Parma ya Italia.

Muda mfupi huko uliishia kwa kurejea Man City kama msaidizi wa Pep Guardiola kwa msimu mmoja, kabla ya kuhamia Leicester miezi kumi iliyopita.








Maresca alishinda tuzo ya Meneja Bora wa Mwezi wa EFL mwezi Agosti kampeni yake ilipoanza vyema, na tuzo hiyo hiyo ikifuatia Oktoba na Desemba.

Mbio bora za Leicester ni mfululizo wa ushindi wa mechi tisa kutoka katikati ya Septemba hadi mwisho wa Oktoba, huku pia wakitoka mechi kumi bila kufungwa kuanzia mwishoni mwa Novemba hadi siku ya mwaka mpya.

Je tutegemee kuona wanachukua ubingwa tena kama walivyofanya msimu wa 2015/16? au wakishiriki na kushuka tena daraja?



# Minong'ono ya usajili duniani



## Leicester kuchangamkia usajili mapema

**LONDON, England**

MABINGWA wa taji la Championship, Leicester City wataweza kusajili wachezaji wakati wa dirisha la usajili la majira ya kiangazi licha ya kuwekewa vikwazo na Bodi ya Ligi ya Soka ya Uingereza kwa kupewa barua yenye masharti kadhaa ambayo yanapaswa kukamilika kwanza kabla ya usajili kuanza.

Hata hivyo, Foxes watalazimika kuuza wachezaji kabla ya Juni 30 ili kuepuka malipo ya sheria ya faida na uendelevu (PSR) msimu ujao huku kiungo wao kati na timu ya taifa ya Uingereza Kiernan Dewsbury-Hall, 25, akizivutia Brentford, Brighton na Fulham.

## Paris wamkatia tamaa Rashford



**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya Paris Saint-Germain wamepunguza nia ya kumnunua Marcus Rashford na watafuatilia kwa karibu kama wataweza kuipata huduma ya kinda huyo au kutafuta mshambuliaji mwingine kabla ya dirisha la kiangazi kupita.


Miamba hao wa Ufaransa wanatafuta mbadala wa Kylian Mbappe baaada ya kutangaza nia ya kuondoka na kutimkia Real Madrid.

## Defoe awania Umeneja Sunderland

**LONDON, England**

MSHAMBULIZI wa zamani wa Uingereza Jermain Defoe, 41, huenda akapata nafasi yake ya kwanza ya kuwa meneja baada ya kufanya mazungumzo na klabu ya zamani ya Sunderland.

Defor alicheza kwa mafaanikio makubwa akitumikioa vilabu kama West Ham United, Tottenham Hotspur, Portsmouth,Toronto FC, Sunderland, AFC Bournemouth pamoja na Rangers.



## Liverpool bado ina malengo na Salah

**LIVERPOOL, England**

LIVERPOOL wanatarajia Mohamed Salah kusalia katika klabu hiyo msimu ujao huku akiingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake uliopo.

Salah ambaye atatimiza umri wa miaka 32 mwezi Juni, atakuwa na jukumu muhimu katika mustakabali wa klabu hiyo chini ya Arne Slot, ambaye anatazamiwa kuthibitishwa rasmi kama mrithi wa Klopp.




*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

# Uelekeo Spoti

| Jumatano Mei 01 - 07, 2024 |

## Zamalek yatinga fainali Shirikisho Afrika




**KUMASI, Ghana**

TIMU ya Zamalek SC ya Misri imefanikiwa kutinga Fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika baada ya ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya wenyeji, Dreams FC Uwanja wa Baba Yara Jijini Kumasi hapa nchini Ghana.

Mabao ya Zamalek yalifungwa na beki Mtunisia, Hamza Mathlouthi dakika ya 12, mshambuliaji Mbenin Samson Akinyoola dakika ya 27 na kiungo Mmisri, Mostafa Shalaby dakika ya 59.

Zamalek inakwenda fainali kwa ushindi huo wa ugenini baada ya sare ya bila kufungana na Dreams kwenye mchezo wa kwanza wiki iliyopita Jijini Cairo Misri na sasa itakutana na RSB Berkane ya Morocco iliyofuzu bila jasho kufuatia mabingwa watetezi, USM Alger kutotokea uwanjani jana Jijini Berkane.

## Mtibwa yamlilia Jamal Byser

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuendelea kupata vipigo mfululizo kwenye Ligi Kuu ya NBC, Klabu ya Mtibwa Sugar ya Turiani Manungu Morogoro imefichua kuwa, hali hiyo inatokana na Mkurugenzi wake wa zamani Jamal Byser kujiweka pembeni na timu yao.

Hayo yamesemwa na Afisa Habari wa Mtibwa Sugar Thobias Kifaru mara baada ya kipigo cha bao 2-1 ilichopata timu yao dhidi ya Mtibwa Sugar juzi kwenye Uwanja wa Meja Generali Isamuhyo Mbweni Jijini Dar es Salaam juzi.

Kifaru akiongea huku akiwataka wadau wa soka kuiombea timu yao, amesema kukosekana kwa watu sahihi wa kuiongoza Mtibwa Sugar tangu kujiweka pembeni kwa Byser ndiyo sababu ya timu yao kufanya vibaya



kwa misimu minne sasa.

"Muendelee kutuombea kwa Mungu, lazima tukiri tunaweza kupotea, haya ni matokeo mabovu mno tunayoendelea kuyapata ambayo yanatokana na kukosa watu sahihii wa kuongoza timu yetu. Viongozi wetu wameshindwa kuvaa viatu vya Jamal Byser," aliongea kwa uchungu Thobias Kifaru.

Juzi wenyeji, JKT Tanzania waliibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Mtibwa Sugar ambapo mabao yao yalifungwa na Edson Katanga dakika ya saba na Sixtus Sabilo dakika ya 90, wakati bao pekee la Mtibwa Sugar lilifungwa na Charles Ilamfya dakika ya 22.

Kwa ushindi huo, JKT Tanzania imefikisha pointi 26 katika mchezo wa 24 na kusogea nafasi ya 10, wakati Mtibwa Sugar inabaki nafasi ya mwisho kwenye Ligi ya timu 16 ikiwa na pointi 17 za mechi 23 sasa.

Huu ni mwaka wa nne mfululizo Mtibwa Sugar inasuasua kwenye Ligi Kuu ambapo baada ya kunusurika kushuka daraja kwenye miaka mitatu iliyopita, bado hali ni ngumu kwao.




# Yanga yapigwa rungu tena na FIFA

## TFF nayo yakazia hukumu

**Na Hamid Yassin**

KABLA Klabu ya Yanga haijatatua adhabu waliyopewa ya kufungiwa kusajili na Shirikisho la Soka Duniani (FIFA) kwa kukiuka kanuni za usajili, Shirikisho hilo limeipiga rungu lingine kwa kupuuza kumlipa mchezaji wao wa zamani, Mzambia Lazarous Kambole aliyeshinda kesi dhidi yao.

Taarifa kutoka Shirikisho la Soka nchini (TFF) iliyotolewa jana imesema kuwa, Yanga imefungiwa kusajili mpaka itakapomlipa Kambole kama walivyotakiwa na FIFA lakini wameshindwa kufanya hivyo kwa wakati waliopewa.

TFF imesema Kambole alifungua madai FIFA akidai malipo ya malimbikizo ya mishahara na fidia ya kuvunjiwa mkataba wake na klabu hiyo. Yanga ilitakiwa iwe imemlipa mchezaji huyo ndani ya siku 45 tangu uamuzi huo ulipotolewa, lakini haikutekeleza hukumu hiyo.

Kutokana na FIFA kuifungia Yanga kusajili Kimataifa, TFF nayo imeipa kibano klabu hiyo kutofanya usajili wa ndani.

Aprili 12 mwezi uliopita TFF ilitoa taarifa ya FIFA kuifungia Yanga kufanya usajili wa kimataifa kwa kukiuka kipengele namba 3 cha kanuni za uhamisho wa wachezaji (RSTP) cha Shirikisho hilo.

Pamoja na mambo mengine ilielezwa kuwa, Yanga haikuingiza uthibitisho wa malipo ya uhamisho wa mchezaji husika (hakutajwa jina) katika mfumo wa usajili (TMS), licha ya kukumbushwa kufanya hivyo.

Yanga ilitakiwa kutekeleza matakwa hayo ya kikanuni na kuwasilisha taarifa kwa Sekretarieti ya Kamati ya Nidhamu ya FIFA ambapo suala hilo lilifikishwa kwa ajili ya hatua zaidi.

Katika hatua nyingine, TFF imezikumbusha klabu kuheshimu mikataba ambayo inaingia na wachezaji na makocha ili kuepuka adhabu mbalimbali ikiwemo kufungiwa.




## Simba sikio la kufa

**Na Mwandishi Wetu**

Kama kuna msemo wa Kiswahili unawafaa Simba msimu huu ni 'Sikio la kufa halisikii dawa' baada ya kuiruhusu Namungo kusawazisha bao dakika ya 89 katiika mechi ya Ligi Kuu ya NBC kwenye Uwanja wa Majaliwa Ruangwa jana.

Kwa matokeo hayo, Simba imeweka rehani nafasi yake ya kushiriki michuano ya kimataifa msimu ujao, kwani inatakiwa ifanye kazi ya ziada kuiondoa Azam FC kwenye nafasi ya pili iliyopo sasa.

Iliwachukua Simba dakika 33 kupata bao lake la kwanza kupitia kwa kiungo mshambuliaji wake Willy Essomba Onana, lakini kama kawaida yao wakaruhusu kirahisi bao hilo kusawazishwa na Namungo dakika sita baadaye baada ya mshambuliaji Kelvine Sabato 'Kongwe' kupiga kichwa katikati ya mabeki wanne wa Wekundu hao wa Msimbazi.

Simba ilipata bao lake la pili dakika ya 70 lililofungwa na kiungo mshambuliaji wa kushoto, Edwin Balua kwa mpira wa adhabu ndogo nje kidogo ya eneo la hatari la Namungo.

Huku mashabiki wengi wakiamini Simba itaondoka uwanjani na alama tatu, lakini wapi haikuwa hivyo, kwani dakika ya 89 Namungo walisawazisha baada ya beki Kennedy Juma kujifunga kufuatia kuchanganyana na kipa wake Ayoub Lackred.